JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

# SERA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MWAKA 2014

Toleo la **2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

# SERA YA ELIMU NA MAFUNZO MWAKA 2014

**Toleo la 2023**

## YALIYOMO

UKURASA


VIFUPISHO .... v
TAFSIRI YA DHANA .... vi
DIBAJI .... vii
SURA YA KWANZA .... 1
UTANGULIZI NA HALI ILIVYO .... 1
1.1. Utangulizi .... 1
1.2. Hali Ilivyo Sasa .... 4
1.2.1. Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu .... 4
1.2.1.1. Elimu Msingi na Elimu ya Ualimu .... 4
1.2.1.2. Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi .... 6
1.2.1.3. Elimu ya Juu .... 6
1.2.2. Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora .... 7
1.2.3. Upatikanaji wa Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo .... 14
1.2.4. Mahitaji ya Rasilimaliwatu .... 18
1.2.5. Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo .... 19
1.2.5.1. Elimu-Msingi .... 19
1.2.5.2. Elimu ya Ualimu na Walimu .... 20
1.2.6. Ushirikiano katika Uendelezaji wa Elimu na Mafunzo .... 21
1.2.6.1. Ushirikiano na Mamlaka za Elimu Zanzibar .... 21
1.2.6.2. Ushirikiano na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa .... 21
1.2.6.3. Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Binafsi .... 22
1.2.7. Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Maendeleo ya Elimu na Mafunzo .... 22
1.2.8. Upatikanaji wa Taarifa na Takwimu Sahihi za Elimu na Mafunzo .... 23
1.2.9. Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo .... 23
1.2.10. Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka .... 24
1.2.10.1. Elimu ya Mazingira .... 24
1.2.10.2. Maambukizi ya VVU na UKIMWI .... 25
1.3. Udhaifu wa Sera katika Utekelezaji Wake .... 26
1.4. Changamoto za Utoaji wa Elimu na Mafunzo .... 26
SURA YA PILI .... 28
UMUHIMU, DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA .... 28
2.1. Umuhimu wa Sera .... 28
2.2. Falsafa ya Elimu .... 29
2.3. Madhumuni ya Jumla ya Elimu na Mafunzo .... 29
2.4. Madhumuni ya Elimu na Mafunzo kwa Kila Ngazi ya Elimu .... 30
2.4.1. Elimu ya Awali .... 30
2.4.2. Elimu ya Msingi .... 31
2.4.3. Elimu ya Sekondari .... 32
2.4.4. Elimu ya Juu .... 32
2.5. Dira, Dhima na Malengo ya Sera .... 33
2.5.1. Dira .... 33
2.5.2. Dhima .... 33
2.5.3. Malengo ya Sera .... 33
2.5.3.1. Lengo la Jumla .... 33
2.5.3.2. Malengo Mahsusi .... 34
SURA YA TATU .... 35
MAENEO, MASUALA NA MATAMKO YA SERA .... 35
3.1. Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu .... 35

3.1.1. Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo ....35
3.1.2. Elimu ya Lazima na Muda wa Elimu na Mafunzo .... 37
3.2. Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo ....39
3.2.1. Fursa za Usawa katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo ....39
3.2.2. Elimu na Mafunzo Jumuishi Ngazi Zote .... 40
3.2.3. Utambuzi na Uendelezaji wa Vipaji na Vipawa ....41
3.3. Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ....42
3.4. Utambuzi wa Watu Waliopata Ujuzi na Maarifa Nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu na Mafunzo43
3.5. Elimu ya Watu Wazima na Endelevu .... 44
3.6. Ubora wa Elimu na Mafunzo ....45
3.6.1. Mitaala ya Elimu na Mafunzo ....45
3.6.2. Uthibiti Ubora wa Elimu na Mafunzo ....47
3.6.3. Elimu ya Sayansi na Teknolojia ....49
3.6.4. Nyenzo, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia .... 51
3.7. Miundombinu katika Taasisi za Elimu na Mafunzo .... 52
3.8. Mazingira Salama, Rafiki na Huduma Muhimu Katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo ....53
3.9. Matumizi ya Lugha katika Mawasiliano .... 55
3.10. Lugha ya Kufundishia ....57
3.11. Upimaji na Tathmini Katika Elimu na Mafunzo .... 58
3.12. Masuala ya Rasilimaliwatu .... 59
3.12.1. Upatikanaji wa Rasilimaliwatu katika Sekta ya Elimu ....59
3.12.2. Upatikanaji wa Rasilimaliwatu Mahiri kwa Ajili ya Sekta Nyingine .... 61
3.13. Menejimenti na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo .... 62
3.13.1. Uongozi, Usimamizi na Uendeshaji Fanisi Katika Sekta ya Elimu ....62
3.13.2. Ushirikiano katika Elimu na Mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ....63
3.13.3. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika Elimu na Mafunzo ....64
3.14. Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Maendeleo ya Elimu na Mafunzo ....64
3.15. Upatikanaji wa Taarifa na Takwimu Sahihi za Elimu na Mafunzo ....65
3.16. Ugharamiaji Endelevu wa Elimu na Mafunzo ....66
3.17. Masuala Mtambuka katika Elimu na Mafunzo ....67
3.17.1. Elimu ya Afya ya Mazingira ....67
3.17.2. Magonjwa na Majanga ....68
3.18. Utafiti na Maendeleo ya Sekta ya Elimu .... 68
3.19. Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Binafsi katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo ....69
SURA YA NNE .... 71
MUUNDO WA KISHERIA .... 71
4.1. Utangulizi ....71
4.2. Sheria za Kusimamia Elimu na Mafunzo .... 71
4.2.1. Mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 ....71
4.2.2. Mapitio ya Sheria Mbalimbali za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara yenye Dhamana ya Elimu72
4.2.3. Mapitio ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288 .... 73
SURA YA TANO .... 74
MUUNDO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI ....74
5.1. Muundo wa Kitaasisi .... 74
5.2. Ngazi ya Taifa ....74
5.2.1. Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Mafunzo .... 74
5.2.2. Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Sekta Nyingine .... 75
5.2.3. Wadau wa Maendeleo ....77

5.2.4. Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia ........ 77
5.2.5. Taasisi na Mamlaka Mbalimbali za Kusimamia Utoaji wa Elimu na Mafunzo ........ 77
5.2.6. Taasisi na Bodi Mbalimbali za Kitaalamu ........ 77
5.2.7. Ngazi ya Mkoa ........ 77
5.2.8. Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa ........ 78
5.2.9. Shule na Vyuo ........ 78
5.2.10. Jamii na Wazazi/Walezi ........ 79
5.3. Ufuatiliaji na Tathmini ........ 79
5.4. Hitimisho ........ 79

# VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| BOHUMATA | Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania |
| CoET | College of Engineering and Technology |
| CoICT | College of Information and Communication Technology |
| EAC | East African Community |
| HESLB | Higher Education Students' Loans Board |
| LAT | Lugha ya Alama ya Tanzania |
| NACTVET | National Council for Technical and Vocational Education and Training |
| NECTA | National Examinations Council of Tanzania |
| REO | Regional Education Officer |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SoED | School of Education |
| TCU | Tanzania Commission for Universities |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TSC | Teachers' Service Commission |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UNESCO | United Nations Educational, Scientific and Cultural Organization |
| VETA | Vocational Education and Training Authority |
| VVU | Virusi vya Ukimwi |

## TAFSIRI YA DHANA

| | |
|---|---|
| Elimu ya Amali | Elimu ya maarifa na ujuzi wa kazi |
| Mfumo nyumbufu | Mfumo wa elimu wenye kutoa fursa anuai, uhuru wa kuchagua mikondo na uhuru wa kutumia njia mbalimbali za kupata elimu na mafunzo |
| Uwili | Mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia utoaji wa elimu kwa njia ya nadharia na vitendo |
| Mazingira salama | Mazingira ambayo yanamwezesha mwanafunzi kupata elimu na mafunzo, na kumwezesha kumaliza mzunguko wa elimu na mafunzo katika ngazi husika |
| Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 | Toleo la kwanza la Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 |

# DIBAJI

Tarehe 22 Aprili, 2021, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, alilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika hotuba hiyo iliyosheheni mambo mengi, Mheshimiwa Rais aliahidi yafuatayo:

*"….tutajielekeza katika kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 na kufanya marekebisho kwenye mitaala iliyopo ili ielekezwe kwenye kutoa elimu ujuzi kulingana na mazingira ya nchi na soko la ajira."*

Kazi ya kufanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ilikamilika mwishoni mwa mwaka 2023. Matokeo ya mapitio haya yalikuwa ni mapendekezo ya kufanya mabadiliko ya kuboresha sera hii badala ya kutunga sera mpya. Baada ya mabadiliko na maboresho tumepata **Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la 2023**. Toleo la 2023 la Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014 iliidhinishwa rasmi na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia kikao cha Baraza la Mawaziri cha tarehe 20 Oktoba, 2023.

Kwa hiyo andiko hili sasa ndiyo Sera ya Elimu na Mafunzo ya Tanzania. Kwa wale wanaohitaji kwenda kwa undani, sera hii inapaswa kuitwa **Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la 2023**. Hata hivyo, kwa urahisi, tunaweza kuiita kwa kifupi **Sera ya Elimu na Mafunzo.**

Mchakato wa kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ulichukua takriban miaka miwili na ulihusisha mambo makuu matatu. **Kwanza,** Wizara kwa kushirikiana na Kamati ya Wataalam ilikusanya maoni kutoka kwa wadau mbalimbali wa elimu. Wadau hawa ni pamoja na walimu, wanafunzi, viongozi wa dini, taasisi zisizo za kiserikali, wamiliki wa shule na vyuo, wanazuoni mbalimbali, makundi yenye mahitaji maalum na kadhalika. Juhudi hizi za kukusanya maoni zilitumia mbinu mbalimbali, ikiwa ni pamoja na kuendesha makongamano, kutumia vyombo vya habari, kuomba maoni kwa barua pepe na kadhalika. Tulipata pia fursa ya kuwapitisha waheshimiwa wabunge mara kadhaa na maoni yao yamezingatiwa. Maoni haya yalichakatwa na kutumika katika kutoa toleo jipya la Sera. **Pili,** Kamati zilipitia taarifa za nchi mbalimbali kuona uzoefu wao. Kamati pia ilitembelea baadhi ya nchi kupata uzoefu kwa undani zaidi. Uzoefu wa nchi nyingine umesaidia sana katika kuandaa toleo jipya la sera. **Mwisho**, Kamati ilifanya uchambuzi wa kitaalam kwa kutumia maoni ya wadau na taarifa za uzoefu wa nchi nyingine.Kupitia chambuzi hizi rasimu mbalimbali ziliandaliwa na kujadiliwa na wadau kupata maoni zaidi ya kuboresha.

Rasimu ya mwisho iliyozingatia uchambuzi wa kitaalam, maoni ya wadau na uzoefu wa nchi nyingine ndiyo iliyowasilishwa kwenye Baraza la Mawaziri na ha  mae kupata idhini ya Rais.

Ni muhimu pia kukumbuka kwamba Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, ambayo ndiyo tumeipitia na kutoa toleo la 2023, ilitungwa baada ya ushirikishwaji mkubwa wadau, na pia kutembelea nchi nyingi kujifunza kutoka kwa wenzetu, zoezi ambalo lilikamilika mwaka 2014. Kwa hiyo toleo hili la 2023 la Sera ni matokeo ya mchakato mrefu wa ushirikishwaji wa wadau mbalimbali.

Wakati juhudi za kupitia Sera zikiendelea chini ya Wizara na kamati maalum, mitaala pia ilikuwa inapitiwa chini ya Taasisi ya Elimu Tanzania. Ili kuoanisha utunzi wa sera na mageuzi ya mitaala, Wizara iliunda pia kamati ya kitaifa ya kusimamia ukusanyaji wa maoni na uchambuzi wa mitaala, na kamati hii ilikuwa ikiwasilisha pia rasimu za mitaala kwenye makongamano ya kujadili sera ili kuhakikisha mwelekeo wa sera ndio unaotoa msukumo wa mwelekeo wa mitaala. Kwa msingi huo, mabadiliko ya mitaala ambayo yamefanyika sambamba na uboreshaji wa sera, yalizingatia sana maoni ya wadau, pamoja na kwamba taratibu za kitaalam, kisheria na kikanuni za mabadiliko ya mitaala zilitumika kukamilisha kazi hii.

Sera ya Elimu na Mafunzo imeleta mageuzi makubwa ya elimu kwa lengo la kujenga raia wenye tafakuri tunduizi na rasilimali-watu iliyoelimika na yenye maarifa, stadi, uwezo na mtazamo chanya katika kuchangia na kuleta maendeleo ya Taifa. Ni vizuri sote tuisome na kuielewa. Wale wote wanaohusika na uongozi na utekelezaji wa masuala ya elimu hapa nchini wanao wajibu wa kuisoma Sera hii, kuielewa vizuri na kuizingatia wakati wote. Kuwa na Sera nzuri na jambo moja na la muhimu. Kutekeleza Sera kikamilifu kwa juhudi na maarifa ni jambo jingine ambalo ni muhimu pia. Sasa tuko katika utekelezaji, kwa hiyo nahimiza sote tuzingatie Sera hii kikamilifu. Katika utekelezaji huu wadau ni pamoja na TAMISEMI, wamiliki wa shule binafsi, taasisi za dini, idara zinazoshughulikia utumishi wa umma, wazazi, wanafunzi, viongozi wa taasisi za elimu na Watanzania wote kwa ujumla.

Prof. Adolf F. Mkenda
**Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia**
Novemba, 2023

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI NA HALI ILIVYO

## 1.1.Utangulizi

Elimu ni nyenzo muhimu sana katika kuhakikisha kuwa Taifa linakuwa na wananchi wenye uwezo wa kuchangia katika maendeleo ya nchi yao. Tangu uhuru mwaka 1961, Serikali ya Tanzania katika nyakati tofauti imechukua hatua mbalimbali za kurekebisha mfumo wa elimu ili kufikia malengo ya maendeleo na kuleta matokeo tarajiwa. Kwa sababu hiyo, sera zinazoongoza elimu zimekuwa zikiboreshwa ili kukidhi malengo ya mfumo wa elimu kwa kipindi husika. Kwa mfano, Wizara ya Elimu ilianzisha Sheria ya Elimu mwaka 1962 kuashiria kuanza kwa mageuzi katika sekta ya elimu ambapo mkazo mkubwa uliwekwa katika kuwaandaa Watanzania kitaaluma ili kujaza nafasi za Serikali zilizokuwa zimechukuliwa na baadaye kuachwa wazi na wageni. Hivyo, sheria ya elimu iliagiza shule zote za msingi kuongeza muda wa programu zao za masomo hadi kufikia miaka minane na kusisitiza umuhimu wa kuongeza upatikanaji wa fursa za elimu ya sekondari.

Mnamo mwaka 1967, mabadiliko katika sera ya elimu yalifanyika kwa kuanzisha Sera ya Elimu ya Kujitegemea iliyotokana na Azimio la Arusha. Sera hiyo ililenga kuleta mageuzi katika sekta ya elimu kwa kushughulikia na kuondoa changamoto mbalimbali za mfumo wa elimu ya kikoloni ambayo ilikuwa bado inatumika katika Tanzania huru. Changamoto za mfumo huo zilijumuisha kuzalisha wasomi kwa ajili ya kazi za ofisini, elimu kuwatenga wanafunzi na jamii zao, na elimu kutoakisi maisha na uchumi wa jamii. Hivyo, sera ya elimu ya kujitegemea ilikusudiwa kurekebisha changamoto bainishwa kwa kuboresha mfumo wa elimu, kubadilisha maudhui ya mitaala, na kurekebisha umri wa watoto kuanza masomo.

Katika kipindi cha utekelezaji wa sera ya elimu ya kujitegemea, masuala mbalimbali yalijitokeza ikiwa ni pamoja na dhana ya elimu na kazi kutokubalika kwa wazazi/walezi, walimu na wanafunzi; kasumba ya mfumo wa elimu ya kikoloni kuwa bado na nguvu katika jamii; na kutojitosheleza kwa elimu ya msingi na sekondari kama ilivyotarajiwa. Matokeo yake ni kuanzishwa kwa Azimio la

elimu ya kujitegemea kwa kufanya mageuzi ya kimkakati kama vile kufanya kazi iwe sehemu ya elimu; kufanya elimu ya msingi kuwa ya lazima na bure kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule; na kurekebisha vigezo vya udahili wa kuingia chuo kikuu. Hata hivyo, mdororo wa uchumi ulioikumba dunia miaka ya 1980, ulisababisha mabadiliko makubwa ya kijamii na kuleta msukumo mpya wa sera ya uchumi huria kufuatia kushindwa kwa sera ya uchumi wa kijamaa. Kwa sababu hizo, Taifa la Tanzania lilihitaji mwelekeo mpya wa kisera katika elimu na mafunzo hasa kufuatia mabadiliko ya sera za jumla.

Mabadiliko hayo ya sera za jumla yalisababisha Serikali kuchukua hatua madhubuti za kuboresha sekta ya elimu katika kipindi cha mwaka 1981-1990. Hatua ya kwanza ilikuwa ni kuanzishwa kwa Tume ya Rais ya Elimu ya mwaka 1981. Tume hiyo iliandaa mapendekezo ya mwelekeo wa baadaye wa mfumo wa elimu na kuteua Kikosi-Kazi cha Kitaifa cha Elimu. Matokeo ya kazi ya Kikosi ni kuwezesha kuandaliwa kwa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995. Aidha Serikali katika kuhakikisha kuwa malengo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 1995 inatekelezwa kwa ufanisi, iliandaa Programu ya Maendeleo ya Sekta ya Elimu ya mwaka 1997. Tangu wakati huo, Wizara ya Elimu imekuwa ikiandaa programu mbalimbali za miaka mitano zenye kuendana na Mipango ya Maendeleo ya nchi na utekelezaji wa Dira ya Taifa. Programu za maendeleo ya sekta ya elimu zilijumuisha Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (2002-2006); Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari (2004-2009); na Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Juu (2005-2010) ambazo ziliongozwa na malengo ya Sera za Elimu.

Mwaka 2014, Serikali ilifanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya 1995; Sera ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya 1996; na Sera ya Taifa ya Elimu ya Juu na hivyo kutunga Sera mpya ya Elimu na Mafunzo. Lengo kuu la Sera hiyo lilikuwa ni kukabiliana na changamoto mbalimbali za elimu na mafunzo zikiwamo changamoto zilizobainika katika mfumo wa elimu na mafunzo; uhaba wa walimu na zana; nyenzo na vifaa pamoja na miundombinu ya kufundishia na kujifunzia; na uwepo wa changamoto za ithibati na uthibiti wa ubora wa shule na vyuo. Kwa sababu hizo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliweka msisitizo katika

kuinua ubora wa mfumo wa elimu na mafunzo ili kuleta tija na ufanisi, kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia usawa na kuendelea kuinua ubora wa mitaala ya elimu na mafunzo ambayo ingekidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa.

Hata hivyo, tangu utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 uanze, wadau wa Elimu wamekuwa wakitoa maoni mbalimbali kuhusu utoshelevu na uhalisia wa maudhui ya Sera katika mitaala ya ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Hoja kubwa za wadau wa elimu ni kuwa maudhui ya sera hii hayajakidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Vilevile, kumekuwa na maoni kwamba kuna mabadiliko mengi yaliyotokea katika nyanja za kisiasa, kiuchumi, kiteknolojia na kijamii ndani na nje ya nchi ambayo bado hayajajumuishwa katika mfumo wa elimu na mafunzo.

Kwa muktadha huo, maoni ya wadau wa elimu pamoja na mabadiliko yaliyotokea, yamedhihirisha uhitaji wa mwelekeo mpya wa Sera ya Elimu na Mafunzo. Kwa sababu hizo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya 2014, Toleo la Mwaka 2023 (Sera), imejumuisha masuala mbalimbali yaliyojitokeza tangu mwaka 2015 yanayolenga kutatua changamoto za kielimu zilizobainishwa ili kuendana na mipango ya kitaifa na mahitaji ya kikanda na kimataifa. Hivyo basi, Sera inatoa mwongozo wa kuimarisha mfumo wa elimu na mafunzo kwa lengo la kutoa fursa anuai za elimu na mafunzo; kutoa elimu yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa; kuandaa rasilimaliwatu ya kutosha na yenye umahiri na weledi unaohitajika kuendana na vipaumbele vya Taifa; na kuimarisha usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini.

Kwa upande mwingine, Sera hii inaendana na maelekezo ya Sera za jumla za kitaifa, makubaliano ya kikanda na kimataifa ambayo yanasisitiza ukuzaji wa maarifa na ujuzi stahiki ili kuongeza tija katika uzalishaji na utoaji huduma. Hivyo, mifumo ya elimu inahitaji kuboreshwa ili kuleta uwiano wa elimu na mahitaji ya soko la ajira kwa kuchochea uvumbuzi, na uhawilishaji wa teknolojia. Vilevile, Sera hii inafungamana na Ilani ya chama tawala kilichounda Serikali. Ilani hiyo imeielekeza Serikali kuzingatia falsafa ya elimu ya kujitegemea inayoendana na mazingira ya nchi yetu, hususan mafunzo ya amali katika kutekeleza wajibu wake wa kuimarisha ubora wa elimu katika ngazi zote.

Aidha, Serikali imesaini na kuridhia itifaki na mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa kuhusiana na masuala ya elimu na mafunzo. Kwa mfano, Malengo Endelevu ya Dunia kuhusu elimu jumuishi yenye ubora na kutolewa kwa usawa; Tamko la Haki za Binadamu kuhusu haki ya elimu kwa wote; *Agenda 2063 - Africa we want* kuhusu elimu jumuishi kwa maendeleo endelevu; na Mkataba wa Uanzishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki - Itifaki ya Soko la Pamoja Ibara ya 11 (*EAC Protocol on Common Market*) na Itifaki ya Elimu na Mafunzo ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (*SADC Protocol on Education and Training)* inayosisitiza uwiano kati ya mifumo ya elimu na mitaala kwa nchi wanachama.

## 1.2. Hali Ilivyo Sasa

### 1.2.1. Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu

Mfumo, miundo na taratibu nyumbufu katika utoaji wa elimu zinatoa fursa kwa wananchi wengi kupata elimu na kuwa huru kutafuta ujuzi katika fani wanayoipenda. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ililenga kuwa na mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo wenye tija na ufanisi na hivyo kuongeza idadi ya wananchi walioelimika na wenye maarifa katika fani mbalimbali, pamoja na kurekebisha muda wa elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali ili kuleta tija, ufanisi na matumizi bora ya rasilimali. Ili kutimiza malengo hayo tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 kuhusiana na hoja ya mfumo na muundo wa elimu ilifanyika, na kubaini mambo yanayoainishwa hapa chini.

#### 1.2.1.1. Elimu Msingi na Elimu ya Ualimu

Kwamba, Mfumo wa Elimu na Mafunzo katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ulilenga kutoa elimu kwa mwaka mmoja kwa watoto wenye umri wa miaka 3-5; na elimu msingi ingetolewa kwa miaka 10, wakati umri wa kuanza darasa la kwanza ulipaswa kuwa kati ya miaka 4–6 kulingana na maendeleo na uwezo wa mtoto kumudu masomo katika ngazi husika.

Tathmini ya utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo 2014 pamoja na maoni ya wadau wa elimu yanaonesha kuwa Serikali ilitekeleza mfumo wa Elimu ya Awali kwa mwaka mmoja kupitia Mwongozo uliozitaka shule za msingi za Serikali kuwa

na darasa la Elimu ya Awali; na sekta binafsi kuanzisha shule za awali. Vilevile, Serikali ilianzisha na kusimamia uendeshaji wa vituo shikizi ili kupunguza umbali ambao watoto walikuwa wakilazimika kutembea kutoka mahali wanapoishi kwenda shule mama. Kutokana na jitihada hizo, kiwango cha uandikishwaji wa wanafunzi wa elimu ya awali kiliongezeka kutoka 1,069,823 mwaka 2015 hadi 1,543,843 mwaka 2022. Idadi hiyo pia ilisababisha kuongezeka kwa wanafunzi wenye elimu ya awali waliojiunga darasa la kwanza kutoka asilimia 76.8 mwaka 2018 hadi asilimia 81.9 mwaka 2022.

Aidha, baada ya kuifanya elimu ya darasa la kwanza hadi kidato cha nne kuwa ya lazima, Serikali iliondoa ada kwa shule za msingi na sekondari kupitia Waraka wa Elimu Na. 3 wa mwaka 2016; na Kidato cha Tano na Sita katika mfumo wa umma kupitia Waraka wa Elimu Na. 5 wa mwaka 2022. Utekelezaji wa afua hizo uliwezesha uandikishaji katika elimu ya msingi kuongezeka kwa asilimia 37.8 kutoka 8,298,282 (4,079,827 wavulana; 4,218,455 wasichana) mwaka 2015 na kufikia 11,420,973 (5,636,996 wavulana; 5,783,977 wasichana) mwaka 2022. Vilevile, wanafunzi waliohitimu darasa VII na kujiunga kidato cha kwanza waliongezeka kutoka asilimia 70.6 mwaka 2015 hadi asilimia 76.6 mwaka 2022.

Hata hivyo, pamoja na juhudi za Serikali za kuimarisha mfumo wa elimu kwa ngazi ya awali, msingi na sekondari, elimu ya msingi imeendelea kuwa ya miaka saba badala ya miaka sita iliyokusudiwa na Sera. Changamoto nyingine ni ukokotoaji wa uandikishaji wa wanafunzi wa rika lengwa kutokana na sera kutoa wigo wa umri wa miaka 3-5 na 4-6 wa kuanza Elimu ya Awali na Darasa la kwanza mtawalia. Vilevile, elimu baada ya elimu ya msingi imeendelea kutawaliwa na utaratibu wa kuchuja wanafunzi kwa ajili ya kuendelea na elimu ya sekondari. Aidha, mfumo uliopo umelenga zaidi kumuandaa mwanafunzi kusoma elimu ya jumla badala ya kutoa fursa anuai za elimu na mafunzo ambazo zingewezesha kumfanya mhitimu kupata ujuzi na maarifa kwa ajili ya ulimwengu wa kazi. Mfumo pia unawanyima wahitimu wengi wa elimu ya msingi na sekondari fursa ya kuendelea na masomo ya ngazi inayofuata ingawa elimu hiyo waliyopata haijawatayarisha vema kushiriki katika ulimwengu wa kazi, yaani kujitegemea. Kwa mfano, takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa takribani asilimia 76.6 ya wahitimu wa darasa la saba

walijiunga na elimu ya sekondari huku asilimia 19.8 tu ya wahitimu wa kidato cha nne wakijiunga na kidato cha tano. Kwa sababu hiyo, mfumo wa elimu unapaswa kuimarishwa kwa kunyumbuliwa zaidi ili kutoa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji na njia mbalimbali za ujifunzaji kulingana na mazingira.

#### 1.2.1.2. Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

Katika kuhakikisha kuwa muda wa kukamilisha elimu na mafunzo katika ngazi mbalimbali baada ya elimu-msingi unatosha kwa mwanafunzi kupata ujuzi stahiki kulingana na mfumo wa tuzo wa Taifa, Serikali iliandaa Mifumo Nyumbufu ya Tuzo ya Tanzania ya Mwaka 2015 ambayo ilihuishwa mwaka 2022. Mifumo hiyo ni pamoja na utoaji tuzo kwa ngazi ya elimu na mafunzo ya ufundi stadi (National Vocational Awards-NVA), mafunzo ya ufundi (National Technical Awards-NTA) na elimu ya chuo kikuu (National University Awards). Mifumo hiyo imewawezesha wahitimu wa ngazi za NVA na NTA kupata ujuzi uliowasaidia kupata fursa mbalimbali za ajira na wengine kujiendeleza katika ngazi za juu za kitaaluma.

#### 1.2.1.3. Elimu ya Juu

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali ilitekeleza afua mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuendeleza programu huria na masafa kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kwa kuanzisha vituo vya mafunzo katika mikoa mbalimbali nchini. Aidha, baadhi ya vyuo vikuu vingine vimeanzisha programu za masafa, huria na changamani kama vile Chuo Kikuu cha Dar es salaam kupitia Ndaki ya Uhandisi (CoET) na Ndaki ya Teknolojia za Habari na Mawasiliano (CoICT) na Shule Kuu ya Elimu (SoED) kwa baadhi ya programu. Kwa kuongezea, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kinatoa programu nne za Stashahada ya Uzamili katika mfumo changamani ambazo ni: Postgraduate Diploma in Education (PGDE), Postgraduate Diploma in Engineering Management (PGDEM), Masters degree in Engineering Management (MEM), and Postgraduate Diploma in Electronics Engineering and Information Technology (PGD-EIT) kupitia vituo vya mikoa ya Mbeya, Mwanza, Dar es Salaam, na Arusha tangu 2007.

### 1.2.2. Elimu na Mafunzo yenye Viwango vya Ubora

Katika kuhakikisha kuwa elimu na mafunzo yanakuwa na viwango vya ubora unaotambulika kikanda na kimataifa na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa, Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ilikusudia kufikia malengo yafuatayo:

i. Kuwa na ufanisi katika uratibu, usimamizi, ithibati na uthibiti ubora katika utoaji wa elimu na mafunzo;

ii. Kuwa na mitaala yenye tija, ufanisi, na inayokidhi mahitaji ya soko la ajira katika kuleta maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani;

iii. Kuwa na idadi ya kutosha ya wananchi walioelimika katika sayansi na teknolojia na kukidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa;

iv. Kuwa na mazingira bora, salama, yenye huduma muhimu na endelevu shuleni na vyuoni ikiwa ni pamoja na huduma ya ushauri na unasihi inayokidhi mahitaji katika elimu na mafunzo;

v. Kuwa na mhitimu mwenye stadi za kudumisha amani, uwezo wa kuhimili na kutatua migogoro katika jamii;

vi. Kujenga uwezo wa kutumia lugha mbalimbali katika mawasiliano na kutumia lugha ya Kiswahili katika ufundishaji; na

vii. Kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi kitaaluma.

Ili kufikia malengo hayo, utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 ulizingatia afua mbalimbali zilizowezesha kuimarisha usimamizi, ithibati na uthibiti wa ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Hivyo, Serikali iliandaa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (2017) kwa ajili ya kutoa mwongozo wa uthibiti ubora, kanuni na viwango vya elimu. Kiunzi hiki pia kiliweka taratibu mbalimbali kwa watendaji katika ngazi ya elimu ya awali, msingi, sekondari, elimu maalumu, elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi na elimu ya ualimu kwenye masuala yahusiyo uthibiti ubora. Mwongozo huo ulifafanua dhana na falsafa ya uthibiti ubora wa elimu; kuimarisha uthibiti ubora wa shule kwa kuongeza idadi ya Wathibiti Ubora wa Shule kutoka 1,179 mwaka 2014 hadi kufikia 1,706 mwaka 2023 ambao walisambazwa katika ngazi za wilaya, kanda na wizara.

Aidha, Serikali iliandaa Mwongozo wa Uanzishwaji na Usajili wa Shule (2020) kwa lengo la kuweka viwango na kuakisi juhudi za wadau mbalimbali na kuhakikisha kwamba elimu inayotolewa nchini inakidhi ubora unaohitajika. Vilevile, Serikali iliandaa Mkakati wa Ujenzi na Ukarabati wa Miundombinu ya Shule za Msingi na Sekondari (2020-2024). Mkakati huo ulikusudia kutoa mwongozo kuhusu misingi, taratibu na viwango vinavyotakiwa katika ujenzi na ukarabati wa shule.

Kwa upande mwingine, taasisi rekebu (taasisi simamizi au elekezi) za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na za elimu ya chuo kikuu zimeimarisha uthibiti ubora wa utoaji wa elimu kwa ngazi husika kwa kuimarisha vitengo vya uthibiti ubora na kutoa mwongozo wa uanzishaji wa vitengo hivyo kwenye taasisi zake. Mathalani, Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) linatumia miongozo ya udahili, usajili wa taasisi na kanuni za uanzishaji wa shahada kwa mujibu wa Tangazo la Serikali (GN. Na. 155) la mwaka 2005. Aidha, Serikali kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali na. 4 ya mwaka 2021 ilihamisha mamlaka ya ithibati ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi kutoka Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) kwenda Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) kwa lengo la kuthibiti ubora wa elimu na mafunzo ya ufundi stadi. Mabadiliko hayo yalibadili muundo wa Baraza na kuitwa Baraza la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (NACTVET) chini ya sheria na. 4 ya mwaka 2021. Zaidi ya hayo, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) pia ilitoa Mwongozo wa Viwango na Vigezo vya Ubora wa Elimu ya Juu mwaka 2019 (*Handbook for Standards and Guidelines for University Education*).

Katika kuhakikisha kuwa mitaala katika ngazi mbalimbali inaendana na wakati na kukidhi mahitaji ya elimu na mafunzo ya sasa na siku zijazo kwa kuzingatia mahitaji ya Taifa, Serikali ilichukua hatua mbalimbali za kuboresha mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote kwa kuzingatia ujuzi uliohitajika. Hivyo, mitaala ya elimu ya awali ilihuishwa mwaka 2016, elimu ya msingi darasa I-VI mwaka 2015, elimu ya msingi darasa I-VII mwaka 2019, elimu ya sekondari Kidato 1-4 mwaka 2010, sekondari Kidato 5-6 mwaka 2009, ualimu astashahada 2009, na elimu maalum mwaka 2019. Hali kadhalika, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi ilianza mwaka 2005 na kuhuishwa kila baada ya miaka mitano ili kukidhi mahitaji

ya soko la ajira ama kuhimili ushindani. Serikali imeendelea kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa kufanya mapitio ya mitaala iliyopo na kuandaa mipya kulingana na mahitaji ya programu za kipaumbele ili ziendane na mahitaji ya soko la ajira.

Kwa muktadha huu, elimu katika Taifa ni muhimili wa kudumisha amani na kujenga stadi za kutatua migogoro, kujenga umoja wa kijamii, utawala bora na mshikamano. Haya yote yalijumuishwa kwenye mitaala.

Kutokana na maendeleo ya teknolojia na mawasiliano, elimu ya sayansi na teknolojia ni nyenzo muhimu katika kumwezesha mwananchi kumudu mazingira yake na kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, ufundishaji wa masomo ya sayansi ulizingatiwa katika ngazi zote ili kupata wataalamu mahiri wa sayansi na teknolojia. Mathalani, masomo yanayohusiana na sayansi na teknolojia kwa shule za msingi yalianza kufundishwa kuanzia darasa la III hadi darasa la VII. Masomo hayo pia yanafundishwa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne huku yakihuishwa kwenye baadhi ya tahasusi za kidato cha 5 na 6. Katika kipindi hiki, Serikali iliweka mkazo kwenye ujenzi wa maabara za sayansi na Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya sayansi na teknolojia.

Kwa upande mwingine, mazingira ya kufundishia na kujifunzia sayansi na teknolojia yameimarishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Kwa mfano, mwaka 2020 shule 1,696 zilipatiwa vifaa vya maabara kwa masomo ya sayansi ambapo kati ya hizo shule 1,625 ni za wananchi na 71 za Taifa. Serikali iliimarisha pia ufundishaji kwa njia ya TEHAMA katika elimu msingi kwa kutoa mafunzo kwa walimu wote tarajali wa vyuo vya ualimu vya Serikali nchini. Katika kuendelea kuimarisha ufundishaji kwa njia ya TEHAMA, Serikali ilinunua na kusambaza kompyuta 1,550 katika vyuo vya ualimu 35 vya Serikali.

Kwa upande wa Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Serikali imeunganisha vyuo 27 kati ya vyuo 32 vya VETA katika mkongo wa Taifa ili kurahisisha mafunzo kwa njia ya TEHAMA. Aidha, idadi ya wanafunzi waliohitimu katika programu za sayansi na teknolojia kwa wastani walikuwa asilimia 16 ya

wahitimu wote kwa mwaka 2020, 2021 na 2022, ambapo mwaka 2020 walikuwa asilimia 16.46, mwaka 2021 asilimia 17.62 na mwaka 2022 asilimia 15.71.

Kwa upande wa elimu ya juu, Serikali imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia masomo ya sayansi na teknolojia kwa kutekeleza yafuatayo: Kujenga na kufanya ukarabati wa miundombinu ya kufundishia ya Taasisi za Sayansi za Bahari - Buyu Zanzibar ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; kujenga maabara mtambuka yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 2,400 kwa wakati mmoja,, kukarabati karakana ya Uhandisi–Kilimo, na kujenga maabara za kemia na baiolojia katika Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa. Matokeo yanaonesha kwamba wastani wa asilimia 24 ya wahitimu wote katika vyuo vikuu wanahitimu katika programu za sayansi na teknolojia ambapo mwaka 2020 wahitimu wa sayansi walikuwa asilimia 24, mwaka 2021 asilimia 27 na mwaka 2022 asilimia 24.4.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali ilichukua hatua mbalimbali kuhakikisha kuwa mitaala inatekelezwa kwa ufanisi. Pia Serikali iliandaa Waraka wa Elimu Na. 4 wa mwaka 2014 kuhusu utayarishaji na upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia. Waraka huo ulihuishwa kwa Waraka Na. 3 wa mwaka 2023 kwa ngazi ya shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vya ualimu. Waraka unalenga kuweka mfumo thabiti wa uhakiki wa maudhui ya vitabu na vifaa vinavyoingizwa na kutumika shuleni ili kuhakikisha vinawajengea wahitimu umahiri na maadili stahiki. Vilevile, Serikali ilinunua na kusambaza vifaa vya maandishi ya breli, vifaa vya kufundishia kuongea (*speech trainer machines*), kipima sauti (*audiometre*) na fimbo nyeupe (*white cane*).

Mafanikio ya afua hizo ni pamoja na Serikali kugharamia uchapaji na usambazaji wa vitabu ambao umewezesha kuongezeka kwa uwiano wa vitabu vya kiada kwa mwanafunzi wa darasa I - VI kufikia wastani 1:3, darasa VII wastani wa 1:1, na sekondari wastani wa 1:3 kwa mwaka 2022. Kwa upande wa taasisi za elimu ya juu, Serikali imejenga na kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia.

Miundombinu hiyo ni toshelevu, salama, rafiki na ni muhimu katika utoaji wa elimu na mafunzo yenye viwango stahiki. Kwa ujumla, miundombinu ya shule, vyuo na taasisi nyingine inajumuisha majengo, mifumo ya maji, na umeme. Zaidi ya hayo, katika kipindi cha utekelezaji wa sera, Serikali imetekeleza afua mbalimbali katika

kuimarisha miundombinu kwa ajili ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote. Afua hizo ni pamoja na kuimarisha mazingira ya kujifunzia na kufundishia kwa kukarabati shule za sekondari za kitaifa 89 zikiwemo shule 07 za ufundi za sekondari ambazo ni Ifunda, Iyunga, Tanga, Mtwara, Moshi, Musoma na Bwiru Wavulana, na kukarabati shule mbalimbali za msingi na sekondari nchi nzima. Serikali imejenga upya vyuo vitano (05) na kukarabati miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika vyuo 30 vya ualimu vya umma. Aidha, Serikali imekarabati vyuo 50 na kujenga upya vyuo vinne (04) vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) na kuvipatia vifaa vya kufundishia/kujifunzia vya kisasa. Vilevile, Serikali imejenga na kukarabati miundombinu ya kufundishia na kujifunzia (madarasa, kumbi za mihadhara, ofisi za wahadhiri, maktaba, mabweni, na maabara) katika Taasisi za Elimu ya Juu ikiwemo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo, Chuo Kikuu cha Dodoma, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam, Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Chu Kikuu Huria cha Tanzania, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya, Chuo Kikuu cha Ardhi, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili, Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Kwa upande wa huduma muhimu, kufikia mwaka 2022 idadi ya shule za msingi za Serikali na zisizo za Serikali 10,793 sawa na asilimia 56 kati ya shule 19,261, na sekondari 4,276 sawa na asilimia 77.2 kati ya shule 5,540 zimeunganishwa na umeme wa gridi ya Taifa.

Katika kuhakikisha uwepo wa mazingira salama na huduma nzuri shuleni na vyuoni, Serikali iliandaa miongozo kadhaa ikiwemo Mwongozo wa Malezi, Unasihi na Ulinzi wa Mtoto kwa Shule na Vyuo vya Ualimu Tanzania (2020); Mwongozo wa Kitaifa wa Utoaji wa Huduma ya Chakula na Lishe kwa Wanafunzi wa Elimumsingi (2020) na Mwongozo wa Kitaifa wa Maji na Usafi wa Mazingira Shuleni (2016).

Masuala ya lugha pia yamezingatiwa katika Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, kwani inasisitiza ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, Sera hii inasisitiza matumizi ya lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika kufundisha na kujifunza hasa shule za msingi, sekondari na vyuo vya ualimu nchini. Katika kipindi cha

utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, lugha ya Kiswahili, Kiingereza, Kichina, Kiarabu na Kifaransa zimeendelea kufundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kama vile Taasisi ya Confusious ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ajili ya kujenga uwezo wa kutumia lugha hizo katika mawasiliano.

Kwa kuongezea, lugha ya Kiswahili na Kiingereza zimeendelea kutumika katika kufundishia na kujifunzia ambapo kwa upande wa elimu ya awali na msingi lugha ya Kiswahili imekuwa ikitumika kufundishia na kujifunzia huku Kiingereza kikitumika kama somo isipokuwa katika baadhi ya shule zilizoruhusiwa kutumia Kiingereza. Lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu. Aidha, lugha ya Kiswahili hutumika kufundishia katika vyuo vya mafunzo ya ualimu ngazi ya astashahada na vyuo vya ufundi stadi. Vilevile, Serikali katika kutekeleza elimu jumuishi iliandaa Kamusi na Mwongozo wa Lugha ya Alama ya Tanzania.

Kwa kuwa upimaji na tathmini ni muhimu katika kubaini maendeleo ya mwanafunzi na changamoto za ufundishaji, ujifunzaji na utekelezaji wa mitaala, Sera ya elimu na mafunzo 2014 ilibainisha hitaji la kuwepo kwa utaratibu wa kitaifa wa upimaji na tathmini katika ngazi na programu mbalimbali za elimu na mafunzo kwa kujumuisha alama za maendeleo ya mwanafunzi na alama za mtihani wa mwisho katika ngazi zote za elimu. Haya yamekuwa yakifanyika katika kipindi cha utekelezaji wa Sera hii.

Aidha, utekelezaji wa afua mbalimbali za kuinua ubora wa elimu na mafunzo Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, uliwezesha kupanda kwa ufaulu katika mitihani ya kitaifa ya darasa la saba kutoka asilimia 57 mwaka 2015 hadi asilimia 82 mwaka 2021; kidato cha nne ufaulu ulipanda kutoka asilimia 68 mwaka 2015 hadi asilimia 87.3 mwaka 2021 na kidato cha 6 kutoka asilimia 98.1 hadi asilimia 99.6 mwaka 2021. Wakati huohuo, wahitimu wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi waliongezeka kutoka 93,247 mwaka 2020 hadi 123,919 mwaka 2021 na Elimu ya Juu kutoka 48,621 mwaka 2020 hadi 54,810 mwaka 2021.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa afua mbalimbali, bado kuna changamoto zinazohusiana na ubora wa elimu na mafunzo. Kwa mfano, uchambuzi wa maoni ya wadau umeonesha kuwa dhana ya ukaguzi wa shule

bado inaendelea kutumika badala ya uthibiti ubora wa elimu yenye kuhitaji ushirikishwaji wa wadau. Vilevile, wataalam katika eneo hili wanakumbwa na changamoto ya upungufu wa maarifa na ubunifu katika kutekeleza dhana ya uthibiti ubora. Kwa sababu hizo, Serikali imeonelea kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha dhana ya uthibiti ubora wa elimu shuleni. Kwa upande wa vyuo vya elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi, elimu ya juu, na uthibiti ubora unakumbana na changamoto ya mwingiliano wa kiutendaji baina ya NACTVET na TCU. Kwa upande mwingine, mazingira ya kufundishia na kujifunzia bado yanakabiliwa na changamoto ya upungufu wa vifaa vinavyohitajika kama vile maabara, maktaba, madarasa, kumbi za mihadhara na samani. Takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kwamba wastani wa uwiano wa darasa kwa wanafunzi katika elimu ya msingi ilikuwa 1:70 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:45; na katika elimu ya sekondari uwiano ulikuwa 1:36 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:35. Wakati huo huo, tathmini ya hali na mahitaji ya miundombinu inaonesha kuwa kwa mwaka 2023 mahitaji ya madarasa ya elimu awali ni 39,058 ambapo yaliyopo ni 5,049, upungufu ukiwa 34,009; kwa shule za msingi mahitaji ya miundombinu ya madarasa ni 216,487 ambapo yaliyopo ni 114,810 na upungufu ni 71,677. Kwa upande wa elimu ya sekondari ya chini (kidato cha 1 - 4), mahitaji halisi ni madarasa 65,481, wakati yaliyopo ni 62,937 na upungufu ni 2,544. Katika ngazi ya vyuo vikuu kuna uhitaji wa kujenga na kukarabati kumbi za semina na mihadhara 130, mabweni 34, maabara 108, ofisi za wahadhiri wa sayansi 55, vyumba vya mikutano ya kisayansi 23 na miundombinu ya mashamba 10 ili kufikia wastani wa uwiano unaohitajika. Hii ina maana kuwa ni muhimu kuwekeza katika miundombinu ya madarasa hasa kwa shule za msingi na sekondari ya chini (Kidato cha 1 - 4), vyuo vya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na vyuo vikuu.

Pamoja na uwepo wa ufaulu mzuri katika mitihani ya ngazi mbalimbali na kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa elimu ya ufundi na elimu ya juu, bado kiwango cha maarifa na ujuzi wa wahitimu katika ngazi hizo ni kidogo ikilinganishwa na ngazi ya elimu waliyofikia. Zaidi ya hayo, maarifa na ujuzi wa wahitimu hao hayakidhi mahitaji mbalimbali katika ulimwengu wa kazi. Kwa sababu hizo, Serikali imekuwa ikisisitiza ufundishaji na matumizi ya sayansi na teknolojia katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Hata hivyo, bado kuna

changamoto ya upatikanaji wa rasilimaliwatu mahiri na wa kutosha, mazingira wezeshi, huduma na vifaa stahiki kwa ajili ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa upande wa lugha bado kuna changamoto ya namna ya ufundishaji wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni kutokana na mahitaji ya Taifa. Changamoto hii inatokana na uhaba wa rasilimaliwatu mahiri na wa kutosha, vifaa na mbinu stahiki za ufundishaji wa masomo ya lugha.

### 1.2.3. Upatikanaji wa Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo

Kila Mtanzania ana haki ya kupata fursa za elimu na mafunzo bila ubaguzi wa jinsi, rangi, kabila, dini, ulemavu na hali ya kijamii au kipato. Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, ililenga kuhakikisha kuwa wanafunzi wote wanakamilisha mzunguko wa elimu katika ngazi husika; kuwa na usawa wa kijinsi katika elimu na mafunzo, kuimarisha elimu na mafunzo kwa kutumia njia mbalimbali ikiwemo ujifunzaji huria na masafa, kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia vipaji, vipawa na kasi ya kujifunza na kutoa fursa ya kuwaendeleza; na kutambua na kurasimisha maarifa, ujuzi na stadi alizopata mtu nje ya mfumo wa shule ili aweze kujielimisha kwa njia mbalimbali.

Tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 imeonesha kuwa Serikali kwa kushirikiana na wadau ilitekeleza afua mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha utoaji wa fursa za elimu na mafunzo kwa usawa. Afua hizo ni pamoja na utoaji wa elimu bila ada kwa shule za awali, msingi na sekondari kupitia waraka wa elimu Na. 3 wa mwaka 2016; Mkakati wa Kitaifa wa Elimu Jumuishi 2021/22-2025/26; Mwongozo wa Kuwarejesha Shuleni Wanafunzi Waliokatiza Masomo Katika Elimu ya Msingi na Sekondari kwa Sababu Mbalimbali wa mwaka 2022; uboreshaji wa miundombinu ya shule za msingi, sekondari, vyuo vya ualimu, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu; programu za elimu kwa njia huria na masafa; Mwongozo wa Utambuzi wa Maarifa na Ujuzi Unaopatikana Nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu; ujenzi wa vyuo vya VETA vya wilaya na mikoa, na ujenzi wa madarasa katika vyuo vya VETA na vyuo vya ufundi; na kuongeza viwango vya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu.

Utekelezaji wa afua hizo umeleta mafanikio ya upatikanaji wa fursa na ushiriki katika elimu na mafunzo. Kwa mfano, idadi ya madarasa ya elimu ya awali imeongezeka kwa asilimia 14.2 kutoka 16,889 mwaka 2015 hadi 19,284 mwaka 2022 na uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 44.3 kutoka 1,069,823 (535,035 wavulana; 534,348 wasichana) hadi 1,543,843 (784,838 wavulana; 759,005 wasichana) mwaka 2022. Uandikishaji katika shule za awali za binafsi umeongezeka kutoka asilimia 8.4 kwa wanafunzi 88,142 (44,974 wavulana; 43,168 wasichana) mwaka 2018 hadi asilimia 9.2 kwa wanafunzi 108,108 (55,364 wavulana; 52,744 wasichana) mwaka 2022. Uandikishaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalumu umeongezeka kutoka 4,171 (wavulana 2,502; wasichana 1,669) mwaka 2016 hadi 6,120 (wavulana 3,575; wasichana 2,545) mwaka 2022.

Pia shule za msingi zimeongezeka kwa asilimia 14 kutoka 16,899 mwaka 2015 hadi 19,261 mwaka 2022. Uandikishaji umeongezeka kwa asilimia 37.8 kutoka wanafunzi 8,298,282 (wavulana 4,079,827; wasichana 4,218,455) mwaka 2015 hadi wanafunzi 11,420,973 (wavulana 5,636,996; wasichana 5,783,977) mwaka 2022. Kwa hiyo, jumla ya wanafunzi 8,011,229 (wavulana 3,934,808; wasichana 4,076,421) waliandikishwa katika shule za Serikali. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wameongezeka kutoka 37,034 (wavulana 21,151; wasichana 15,883) mwaka 2016 hadi wanafunzi 66,372 (wavulana 37,830; wasichana 28,542) mwaka 2022.

Kwa upande wa elimu ya sekondari, uandikishaji sekondari ya chini (kidato cha 1-4) umeongezeka kutoka 1,675,593 (wavulana 824767; wasichana 850,826) mwaka 2016 hadi 2,645,115 (wavulana 1,248,118; wasichana 1,396,997) mwaka 2022 na kidato cha 5-6 kutoka 131,362 (wavulana 81,129; wasichana 50,233) mwaka 2016 hadi 178,473 (wavulana 99,101; wasichana 79,372) mwaka 2022. Aidha, ili kutoa fursa kwa wanafunzi walioacha shule kwa sababu mbalimbali, Serikali imewezesha kuwarejesha wanafunzi 8,652 masomoni, ambapo wanafunzi 6,685 (wasichana) walirejea kupitia utaratibu wa elimu nje ya mfumo rasmi, na wanafunzi 1,967 (wavulana 861; wasichana 1,046) walirejea katika mfumo rasmi wa elimu kwa mwaka 2022/23. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu wameongezeka kutoka 7,512 (wavulana 3,920; wasichana 3,592) mwaka 2016 hadi wanafunzi 13,142

(wavulana 6,422; wasichana 6,720) mwaka 2022. Vilevile, jumla ya wanafunzi 23,263 (wavulana 8,257; wasichana 15,006) wamedahiliwa katika elimu ya sekondari kwa njia mbadala kwa mwaka 2022/23.

Kwa upande wa Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, vyuo vimeongezeka kutoka 716 mwaka 2019/20 hadi 830 mwaka 2020/21. Ongezeko hilo la vyuo limesababisha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaojiunga na elimu na mafunzo ya ufundi stadi kutoka 119,184 (wavulana 80,050; wasichana 39,134) mwaka 2017/18 hadi 380,748 (wavulana 225,621; wasichana 155,127) mwaka 2020/21. Wakati huo huo, vyuo vya elimu ya ufundi vimeongezeka kutoka 429 mwaka 2021 hadi 465 mwaka 2022, na kuongeza udahili kutoka 128,940 (wavulana 68,973; wasichana 59,967) mwaka 2017/18 hadi 179,518 (wavulana 91,995; wasichana 87,523) mwaka 2021/22. Wanafunzi wenye mahitaji maalumu katika vyuo vya ufundi wameongezeka kutoka 108 (wavulana 56; wasichana 52) mwaka 2016 hadi wanafunzi 13,142 (wavulana 6,422; wasichana 6,720) mwaka 2022.

Kwa upande wa vyuo vikuu na vyuo vikuu vishiriki, vilivyosajiliwa kwa mwaka 2015/16 vilikuwa 53 (vya Umma 12 na Binafsi 41); na mwaka 2022 vilikuwa 54 (vya Umma 21 na Binafsi 33) sawa na ongezeko la vyuo vya Serikali 9. Vilevile, kumekuwa na ongezeko la usajili wa wanafunzi kutoka 225,330 mwaka 2015/16 (wavulana 146,322; wasichana 79,008) kufikia wanafunzi 240,523 kwa mwaka 2022/23 (wavulana 133,152; wasichana 107,371). Kati ya waliosajiliwa kwa mwaka 2022/23, jumla ya wanafunzi 1,498 (wavulana 797; wasichana 701) walikuwa wenye mahitaji maalum.

Hata hivyo, pamoja na jitihada zilizofanyika za kuongeza fursa za elimu na mafunzo kwa ngazi mbalimbali, takwimu za sensa za mwaka 2022 zinaonesha kuwa idadi ya watoto wenye umri wa rika lengwa wa elimu ya awali ilikuwa milioni 1.73 mwaka 2022, sawa na asilimia 2.9 ya idadi ya watu wote nchini ambapo ni milioni 1.54 tu sawa na asilimia 89 ya watoto hawa waliandikishwa. Hii ina maana kuwa, pamoja na juhudi za Serikali na wadau, asilimia 11 ya watoto waliostahili kuanza elimu ya awali hawakuandikishwa katika ngazi husika. Kwa upande mwingine, idadi ya watoto wenye umri wa kuanza shule ya msingi (miaka 7-13)

ilikuwa milioni 11.8, sawa na asilimia 19 ya watu wote, huku walioandikishwa wakiwa milioni 11.4 sawa na asilimia 97. Hata hivyo, uandikishaji bila kuzingatia umri lengwa kwa mwaka 2022 ulikuwa asilimia 108.5. Hii ina maana kwamba pamoja na uandikishaji wa jumla wa watoto, bado asilimia 3 ya watoto wenye umri wa kwenda shule hawakuandikishwa. Vilevile, idadi ya watoto wenye umri wa kuanza elimu ya sekondari Kidato cha 1- 4 (miaka 14-17) ilikuwa milioni 5.3, sawa na asilimia 8.8 ya watu wote, huku milioni 2.6, sawa na asilimia 51 ya walengwa wakiandikishwa kwa mwaka 2022. Uandikishaji wa wanafunzi wa jumla kwa kidato cha 1-4 ulikuwa asilimia 48.2 mwaka 2022. Hii inamaanisha kwamba kuna idadi kubwa ya vijana wenye umri wa kuanza elimu ya sekondari ya chini (Kidato 1- 4) ambao bado hawakupata fursa hiyo.

Kwa dhana ya utoaji wa elimu ya amali, Serikali imekuwa ikizingatia utoaji wa elimu ya jumla kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali kuanzia darasa la VII, kidato cha 4 na kidato cha 6. Hata hivyo, kutokana na uhitaji wa ujuzi kwa wahitimu wa ngazi mbalimbali katika soko la ajira, fursa za utoaji wa elimu ya amali zinahitaji kuongezeka katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

Kwa upande wa elimu ya juu, ushiriki mdogo wa wanawake katika baadhi ya programu za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati unaendelea kuonekana licha ya ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi. Kwa mfano, katika programu za uhandisi, uwiano wa mwanamke na mwanamume ni 1 kwa 5. Hivyo, ni muhimu kuweka mazingira wezeshi kwa wanawake kushiriki katika programu za sayansi, teknolojia, uhandisi na hisabati katika elimu ya juu. Vilevile, kuongezeka kwa uhamaji wa wanafunzi katika zama za utandawazi kumeiwezesha Tanzania kunufaika na uingiaji wa wanafunzi wa kimataifa katika taasisi za elimu ya juu. Kwa kutambua umuhimu wa wanafunzi wa kigeni katika taasisi za elimu ya juu, mojawapo ya maeneo ya kimkakati ya msukumo kwa Serikali ni kuifanya elimu ya juu kuwa ya kimataifa.

Kwa kuongezea, tathmini na maoni ya wadau mbalimbali yameonesha kuwa taasisi za elimu ya juu zilirekodi upungufu wa asilimia 19.4 katika udahili wa wanafunzi wa kigeni kutoka 1,170 (747 Raia wa EAC; 423 Raia Wengine) mwaka 2021/22 hadi 943 (560 Raia wa EAC; 383 Raia Wengine) mwaka 2022/23. Raia

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) walikuwa ni asilimia 59.4 ya wanafunzi wote wa kigeni huku asilimia 40.6 wakitoka mataifa mengine. Taarifa zinaonesha kuwa Tanzania imekuwa ikidahili idadi ndogo ya wanafunzi wa kigeni katika elimu ya juu ikilinganishwa na nchi nyingine. Kwa mfano, kwa mwaka 2022, udahili wa wanafunzi wa kigeni ulikuwa asilimia 0.4 ya jumla ya usajili. Asilimia hiyo ni ndogo ikilinganishwa na lengo la SADC la asilimia 5 ya nafasi za kujiunga kwa wanafunzi kutoka mataifa ya SADC. Hii ina maana kuwa juhudi za pamoja za kuimarisha uunganishaji wa kimataifa wa elimu ya juu nchini Tanzania zinahitajika sana.

### 1.2.4. Mahitaji ya Rasilimaliwatu

Rasilimaliwatu ni nyenzo muhimu sana katika kusukuma maendeleo endelevu ya sekta mbalimbali nchini na duniani kote. Katika kutekeleza hilo, Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ililenga kuwa na rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya sekta ya elimu na mafunzo pamoja na sekta nyingine kwa maendeleo ya Taifa.

Kwa mantiki hiyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Serikali ilitekeleza afua mbalimbali kuwezesha upatikanaji wa rasilimaliwatu kwa ajili ya sekta ya elimu na sekta nyingine. Afua hizo ni pamoja na Mkakati wa Upangaji wa Walimu wa Shule za Awali na Msingi kwa kuzingatia Mahitaji (Pre-Primary and Primary Teacher Deployment Strategy 2019 – 2021), Mwongozo wa Walimu wa Kujitolea katika Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Tanzania Bara 2023, kutoa ajira na mafunzo kwa walimu, wakufunzi na wanataaluma pamoja na Mkakati wa Kitaifa wa Maendeleo ya Ujuzi (National Skills Development Strategy - NSDS 2016/17 - 2025/26).

Utekelezaji wa afua hizo umewezesha kuleta mafanikio kadhaa. Kwanza wahitimu wa fani mbalimbali katika vyuo vikuu wameongezeka kutoka 46,294 mwaka 2016/17 hadi 57,742 mwaka 2021/22. Pili, wahitimu wa fani mbalimbali za elimu ya ufundi wameongezeka kutoka 114,656 mwaka 2016/17 hadi 123,919 mwaka 2021/22. Tatu, wahitimu wa mafunzo ya ufundi stadi mwaka 2016/17 walikuwa 111,025 na mwaka 2021/22 walikuwa 147,767. Wahitimu wa astashahada na stashahada kutoka vyuo vya ualimu waliongezeka kutoka 10,427 mwaka 2016/17

hadi 19,193 mwaka 2021/22. Ingawa idadi ya wahitimu wa fani mbalimbali imeongezeka, bado wadau wakiwemo waajiri wamelalamikia kukosekana kwa umahiri unaohitajika kuendana na mahitaji ya soko la ajira. Vilevile, baadhi ya wahitimu wanaozalishwa katika fani na ngazi mbalimbali wameshindwa kuajiriwa na hata kujiajiri.

Katika dhana ya utoshelevu wa rasilimaliwatu iliyopo, kwa mwaka 2022, walimu kwa ngazi ya shule za msingi walikuwa 201,672 na mahitaji yalikuwa 253,799, na hivyo kulikuwa na upungufu wa walimu 52,127 kwa mujibu wa viwango vinavyohitajika. Kwa upande wa sekondari, kwa mwaka 2022, walimu walikuwa 113,205 kwa ujumla ingawa kulikuwa na upungufu wa walimu wa masomo ya sayansi, hisabati na amali. Kwa upande wa Elimu ya Ufundi, kwa mwaka 2022, walimu walikuwa 10,948 sawa na upungufu wa walimu 10,052. Kwa upande wa vyuo vikuu vya umma, wanataaluma walikuwa 3,839 kwa mwaka 2021 ambapo upungufu wa jumla ulikuwa 5,748, yaani Profesa (Professors) 741, Profesa Washiriki (Associate Professors) 671, Wahadhiri Waandamizi (Senior Lecturers) 1,350, Wahadhiri (Lecturers) 1,140 na Wahadhiri Wasaidizi (Assistant Lecturers) 1,846 kwa vyuo vikuu vya Umma.

### 1.2.5. Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo

#### 1.2.5.1. Elimu-Msingi

Usimamizi na uendeshaji madhubuti wa sekta ya elimu na mafunzo nchini unahitaji uongozi imara, na uwajibikaji wenye ufanisi na tija. Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, ililenga kuwa na uongozi, usimamizi na uendeshaji wenye tija na wenye kuimarisha uwajibikaji katika sekta ya elimu na mafunzo; kuimarisha ushirikiano na uhusiano wa kielimu kati ya Tanzania Bara na Zanzibar; kuweka utaratibu wa kutekeleza mahusiano na mashirikiano ya kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo; na kutenga ardhi kwa ajili ya elimu na mafunzo.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali imeendelea na mfumo wa usimamizi na uendeshaji wa elimu kama ilivyokuwa kabla ya Sera hiyo. Kwa ngazi ya Taifa, wizara yenye dhamana ya elimu imeendelea na jukumu la kuandaa sera ya elimu na maendeleo ya mafunzo,

pamoja na utekelezaji wake nchini, wakati Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR – TAMISEMI) ikiwa na jukumu la kusimamia sera ya ugatuaji wa madaraka kwenda ngazi ya chini ambako ndiko utekelezaji wa sera ya elimu unakofanyika, kusimamia tume ya utumishi wa walimu; na uendeshaji wa elimu ya msingi na sekondari.

Kutokana na mfumo kuendelea kama ulivyokuwa hapo awali, kumekuwa na mwingiliano wa kiutendaji kwa baadhi ya majukumu kati ya wizara yenye dhamana ya elimu, na OR – TAMISEMI. Hali hii imesababisha kuendelea kuwepo kwa changamoto za kiutendaji. Hivyo, kuna umuhimu wa kuboresha utendaji wa vyombo vya wizara yenye dhamana ya elimu na majukumu ya OR-TAMISEMI katika usimamizi na uendeshaji wa masuala ya elimu.

#### 1.2.5.2. Elimu ya Ualimu na Walimu

Usimamizi wa mafunzo ya walimu yanayotolewa kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada katika vyuo vya ualimu yanasimamiwa na Wizara ya Elimu. Kwa ngazi ya shahada, mafunzo yanatolewa na vyuo vikuu chini ya usimamizi wa TCU. Kwa utaratibu huo, vigezo vya elimu ya ualimu vinawekwa na mamlaka mbili tofauti, yaani TCU na vyuo bila kuhusiana katika ithibati na uthibiti wake.

Kwa upande mwingine, walimu na taaluma ya ualimu vinasimamiwa na vyombo viwili pia ambapo kuna Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) iliyoanzishwa kupitia Sheria ya Tume ya Utumishi wa Walimu, Sura ya 448, na Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania kupitia Sheria ya Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania, Sura ya 314. Tume ya Utumishi wa Walimu inasimamia utumishi wa walimu ikiwemo kuajiri, kutawanya, kutengeneza rejista ya walimu na kupandisha vyeo. Bodi ya Kitaalamu ya Walimu Tanzania inasimamia utaalamu wa ualimu nchini kwa walimu wote. Uwepo wa vyombo hivi viwili umeleta mwingiliano wa majukumu na hivyo kuna umuhimu wa kuboresha usimamizi wa walimu na taaluma ya ualimu kuwa chini ya chombo kimoja kitakachosimamia mambo yote.

### 1.2.6. Ushirikiano katika Uendelezaji wa Elimu na Mafunzo

#### 1.2.6.1. Ushirikiano na Mamlaka za Elimu Zanzibar

Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Sura ya 2, inatambua masuala ya Elimu ya Juu na Baraza la Taifa la Mitihani la Tanzania (NECTA) na mambo yote yanayohusika na kazi za Baraza hilo kuwa ni ya Muungano. Aidha, ngazi nyingine za elimu ikiwa ni pamoja na elimu ya msingi, sekondari, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi si sehemu ya masuala ya Muungano. Hata hivyo, Serikali za pande zote mbili za Muungano zinashirikana katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya elimu hasa katika yale ya mitaala na upimaji kwa ngazi ya sekondari na elimu ya ufundi.

Ushirikiano huu unaendelezwa kupitia baadhi ya taasisi na vyuo vya elimu ya juu ambavyo vimefungua matawi yake Zanzibar. Baadhi ya taasisi hizo ni Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB), Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania. Serikali inaona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha ushirikiano katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

#### 1.2.6.2. Ushirikiano na Mashirika ya Kikanda na Kimataifa

Ili kuboresha usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini, Serikali imeendelea na ushirikiano na mashirika ya kikanda na kimataifa katika masuala ya maendeleo ya elimu na mafunzo. Ushirikiano huo unaongozwa na mikataba mbalimbali kama vile Commonwealth of Learning (COL), SDG’s, Agenda 2063 - Africa We Want, Unesco-Perth Declaration (2007), SADC na EAC. Pia kumekuwa na ushirikiano baina ya Tanzania na nchi mbalimbali pamoja na uanzishwaji wa jukwaa la Mamlaka ya Udhibiti wa Ufundishaji la Afrika (Africa Forum of Teaching Regulatory Authority – AFTRA).

Pamoja na mafanikio katika kutekeleza mahusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa, bado kuna changamoto ya utekelezaji wa baadhi ya makubaliano kama vile Itifaki ya Soko la Pamoja kwa Uwianishaji wa Mifumo ya Elimu na Mitaala ya Elimu na Mafunzo, Utambuzi wa Pamoja wa Sifa za Kitaaluma na Kitaalamu kwa

Jumuiya ya Afrika Mashariki, Azimio la Eneo Moja la Elimu ya Juu kwa Afrika Mashariki la mwaka 2017, na baadhi ya makubaliano kati ya Tanzania na nchi mbalimbali. Aidha, hakuna mpango madhubuti wa utekelezaji wa makubaliano haya ya kikanda na kimataifa.

#### 1.2.6.3. Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Binafsi

Sekta ya elimu ni eneo muhimu la ushirikiano baina ya sekta ya umma na binafsi ambapo sekta hizi zinashiriki kutoa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali imekuwa ikishirikisha wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, jamii, wadau wa maendeleo, mashirika na taasisi binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo. Ushirikiano huo ulihusisha ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya shule na vyuo, utoaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia, utoaji wa mafunzo kwa walimu, utoaji wa huduma ya afya, chakula na lishe, maji, mawasiliano, uendeshaji wa shule na vyuo na uchangiaji wa bajeti ya Serikali.

Pamoja na mchango mkubwa wa wadau mbalimbali katika utoaji wa elimu na mafunzo, bado sekta ya elimu inahitaji kuongeza ushiriki wa wadau kwa njia mbalimbali ikiwemo utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote.

### 1.2.7. Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Maendeleo ya Elimu na Mafunzo

Mahitaji ya ardhi kwa ajili ya ujenzi, upanuzi na uendelezaji wa taasisi za elimu na mafunzo yanaendelea kuongezeka kutokana na azma ya Serikali kuongeza fursa za elimu na mafunzo katika ngazi zote. Kwa mantiki hiyo, katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali kupitia mipango ya matumizi ya ardhi katika Mamlaka za Zerikali za Mitaa imekuwa ikitenga maeneo kwa ajili ya uanzishaji na uendelezaji wa mipango ya elimu na mafunzo. Hata hivyo, baadhi ya maeneo yaliyotengwa yamekuwa yakivamiwa na wananchi kwa ajili ya shughuli binafsi na mengine kubadilishiwa matumizi. Hali hii inatokana na baadhi ya taasisi na asasi za elimu kutokuwa na hati miliki za maeneo husika. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha ulinzi wa maeneo yaliyotengwa kwa

ajili ya utoaji wa huduma za elimu na mafunzo kwa kuhakikisha taasisi za elimu na mafunzo zinapata hatimiliki za maeneo yao ya ardhi na Serikali kulinda maeneo hayo dhidi ya uvamizi.

### 1.2.8. Upatikanaji wa Taarifa na Takwimu Sahihi za Elimu na Mafunzo

Sekta ya elimu na mafunzo inahitaji kuwa na mfumo wa kupata na kutoa taarifa za utendaji kwa wadau wake. Mfumo huo unahitaji kuwa madhubuti ili ukusanyaji, uchakataji, utunzaji na usambazaji wa taarifa uwe sahihi na wa kuaminika na unaowezesha taarifa kupatikana kwa wakati. Kwa sasa, mifumo mingi ya kielimu imeunganishwa na mifumo mingine ya taarifa za Serikali. Kwa mfano, mfumo wa udahili wa vyuo vikuu, vyuo vya ufundi, vyuo vya ualimu na mfumo wa matokeo ya Baraza la Mitihani la Taifa la Tanzania, mfumo wa vizazi na vifo, yote imeunganishwa. Hata hivyo, baadhi ya taarifa muhimu zimewekwa katika mpangilio tofauti tofauti na hivyo kusababisha kuchelewa kwa upatikanaji wa taarifa muhimu za kisekta kwa ajili ya matumizi kulingana na mahitaji.

### 1.2.9. Mfumo Endelevu wa Ugharimiaji wa Elimu na Mafunzo

Sekta ya elimu ni moja ya sekta muhimu na za kipaumbele cha juu. Kwa kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali ililenga kuwa na mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo, kwa sababu Serikali imeendelea kugharamia elimu na mafunzo kwa kushirikiana na wazazi, jamii na wadau wengine wa maendeleo wa ndani na nje. Ugharimiaji huo unahusisha ujenzi wa miundombinu, ununuzi wa vifaa, nyenzo na zana za kufundishia na kujifunzia pamoja na uendeshaji wa shule na vyuo kwa ngazi mbalimbali. Hivyo, bajeti ya Serikali kwa sekta ya elimu imekuwa ikiongezeka kutoka trilioni 4.77 mwaka 2016/17 hadi trilioni 5.26 mwaka wa fedha 2021/22.

Licha ya ongezeko la bajeti la kila mwaka, bado kuna changamoto katika ugharimiaji wa elimu na mafunzo nchini. Changamoto hizo ni pamoja na fedha zilizotengwa katika bajeti ya Serikali kutotosheleza mahitaji ya elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu. Hali hii imeathiri ubora wa elimu na mafunzo yatolewayo nchini kwani inasababisha upungufu wa miundombinu na uhaba wa

vifaa vya kufundishia na kujifunzia kama vile vitabu, maabara, maktaba, madarasa, na kumbi za mihadhara. Kwa mfano, mwaka 2022, uwiano wa kitabu kwa mwanafunzi katika elimu ya msingi ulikuwa 1:2 na elimu ya sekondari 1:3, ukilinganisha na uwiano unaotakiwa wa 1:1. Pia, wastani wa uwiano wa darasa kwa wanafunzi katika elimu ya msingi ulikuwa 1:70 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:45; huku elimu ya sekondari ikiwa na uwiano wa 1:36 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:35. Uwiano wa sekondari, angalau, umefikia kiwango cha kuridhisha.

Hali hiyo imetokana na jitihada za uwekezaji wa Serikali katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Kwa mfano, wahitimu wa elimumsingi wameongezeka sana. Hii imeongeza umuhimu wa kuongeza uwekezaji katika ngazi zote ikiwemo elimu ya juu. Kwa msingi huo, kuna umuhimu wa kuimarisha mfumo wa ugharimiaji wenye vyanzo anuai na endelevu kwa ajili ya elimu na mafunzo katika ngazi zote.

### 1.2.10. Mfumo wa Elimu na Mafunzo Unaozingatia Masuala Mtambuka

Mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka ulilenga kuwa na wahitimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo wenye maarifa, stadi na utamaduni wa kutunza mazingira; kutoa elimu kwa wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla ili kupunguza kasi ya kuenea kwa maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) na Ukosefu wa Kinga Mwilini (UKIMWI); na kuongeza uwezo wa sekta ya elimu na mafunzo katika kupanua na kuimarisha miundombinu na huduma zinazotolewa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

#### 1.2.10.1. Elimu ya Mazingira

Elimu ya mazingira ni moja ya nyenzo muhimu katika kuhakikisha uwepo wa afya bora na mazingira salama na wezeshi kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Katika kipindi cha utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali ilizingatia masuala ya mazingira katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote. Elimu ya mazingira imezingatiwa katika malengo na maeneo ya ujifunzaji katika mitaala ya elimu ya awali hadi kidato cha 5 na 6. Kwa upande wa elimu ya juu, kuna programu maalumu za elimu ya sayansi na mazingira zinazofundishwa.

Kwa kiasi kikubwa, utekelezaji wa ufundishaji wa elimu ya mazingira umeleta matokeo chanya katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Hata hivyo, kuongezeka kwa idadi ya watu kumeongeza uhitaji wa huduma au shughuli mbalimbali za kijamii na kiuchumi ambazo kwa kiasi kikubwa zinakiuka taratibu za uhifadhi na kuchangia katika uharibifu wa mazingira nchini. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa kuimarisha na kupanua uwanda wa utoaji wa elimu ya mazingira katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

### 1.2.10.2. Maambukizi ya VVU na UKIMWI

Sekta ya elimu ni mojawapo ya sekta zinazoathiriwa na magonjwa mbalimbali ikiwa ni pamoja na VVU na UKIMWI. Magonjwa hayo yamechangia mahudhurio duni kutokana na kuugua kwa muda mrefu na udhaifu kwa baadhi ya walimu na wanafunzi katika taasisi za kielimu, hivyo kuathiri maendeleo ya taaluma. Katika kipindi cha utekelezaji wa sera, masuala ya VVU na UKIMWI yalizingatiwa katika mitaala ya ngazi zote za elimu na mafunzo. Mfano, katika somo la uraia na maadili, na sayansi na teknolojia, mada ya VVU na UKIMWI imekuwa ikifundishwa katika ngazi ya elimu ya msingi.

Kwa ngazi ya elimu ya sekondari, mada hiyo hufundishwa kwenye somo la Uraia na Baiolojia. Aidha, taasisi za elimu na mafunzo zinaendelea kutoa huduma kwa wafanyakazi wanaoishi na VVU na UKIMWI kwa kuzingatia mwongozo wa kudhibiti VVU, UKIMWI na magonjwa sugu yasiyoambukiza katika utumishi wa Umma wa mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha afya, kinga, uelewa sahihi kuhusu chakula na lishe, uangalizi wa karibu, mazingira wezeshi, matibabu na huduma kwa wanaoishi na VVU na UKIMWI.

Hata hivyo, pamoja na mitaala kusisitiza utoaji wa elimu ya VVU na UKIMWI katika ngazi zote, changamoto ya mitaala kutotilia mkazo wa utoaji wa elimu kuhusu magonjwa mengine yanayoambukiza na yasiyoambukiza ambayo yana athari katika utoaji wa elimu na mafunzo imeendelea kushamiri. Hivyo, kuna umuhimu wa kuzingatia utoaji wa elimu ya magonjwa mengine ambayo hayakupewa kipaumbele au msisitizo katika utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014.

## 1.3. Udhaifu wa Sera katika Utekelezaji Wake

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, ulikumbwa na changamoto kama vile:

(i) *Baadhi ya maeneo ya sera kukosa ufafanuzi wa kutosha*

Hali hii ilitoa mwanya wa tafsiri tofauti katika baadhi ya maeneo ya msingi kama vile muundo wa elimu, ujuzi uliokusudiwa, lugha ya kufundishia, kutokuwa na umri mahsusi wa kuanza elimu ya awali na elimu ya msingi kwa kutambua kuwa watoto hustahili kupata fursa ya malezi na makuzi ya awali ya watoto wadogo;

(ii) *Baadhi ya maeneo ya sera kutotekelezwa*

Maeneo hayo ni kama: mfumo wa elimu ya lazima wa miaka kumi kutotekelezeka; kukosekana kwa muundo wa kutekeleza uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo; kutokuwepo kwa sheria ya elimumsingi na sekondari; kukosekana kwa utaratibu wa kuwezesha maendeleo ya wanafunzi wenye vipaji, vipawa na kasi tofauti na mahitaji maalum; na kukosekana kwa utaratibu na utambuzi wa maarifa, ujuzi, na stadi zilizopatikana nje ya mfumo rasmi wa shule; na

(iii) *Baadhi ya maeneo muhimu kutozingatiwa kwenye sera*

Maeneo hayo ni elimu ya ualimu, elimu ya juu, utafiti katika elimu na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa elimu na mafunzo. Aidha, maeneo mengine yalihusu malengo ya jumla ya elimu na malengo kwa kila ngazi ya elimu na mafunzo bila malengo mahususi.

## 1.4. Changamoto za Utoaji wa Elimu na Mafunzo

Jukumu kuu la sekta ya elimu ni kuzalisha nguvukazi ya kutosha na yenye umahiri na weledi stahiki katika ngazi mbalimbali na katika uwiano stahiki kwa maendeleo ya Taifa. Katika jitihada za kutekeleza jukumu hilo, sekta ya elimu inakabiliwa na changamoto mbalimbali, kama vile:

(a) Mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji na njia mbalimbali za ujifunzaji

kulingana na mazingira;

(b) Mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia;

(c) Mfumo usio na ufanisi wa uthibiti na ithibati ya elimu na mafunzo katika ngazi zote;

(d) Upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali;

(e) Mfumo dhaifu wa usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo;

(f) Mfumo usio wa uhakika na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu; na

(g) Kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

## SURA YA PILI

## UMUHIMU, DIRA, DHIMA NA MALENGO YA SERA

### 2.1. Umuhimu wa Sera

Uchambuzi wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 umebaini kuwa sera hiyo ililenga kutekeleza malengo saba - mfumo, muundo na taratibu nyumbufu kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu; elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa; upatikanaji wa fursa mbalimbali za elimu na mafunzo nchini; ongezeko la rasilimaliwatu kulingana na vipaumbele vya Taifa; usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini; mfumo endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo nchini; na mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka.

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa sera, bado malengo hayo ni muhimu katika muktadha wa sasa kwa kuzingatia changamoto zilizobainishwa kama vile mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji; njia mbalimbali za ujifunzaji kulingana na mazingira; mitaala ya elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia; kuwa na mfumo usio fanisi wa uthibiti na ithibati ya elimu na mafunzo katika ngazi zote; upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali; kukosekana kwa mfumo madhubuti wa usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo; kukosekana kwa mfumo anuai wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo endelevu; na kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

Kwa kuzingatia hali hiyo, baadhi ya maeneo ya sera yanatakiwa kuendelea kuwepo na kuboreshwa ikiwemo kuyatolea ufafanuzi ili yaeleweke zaidi na yaendane na mazingira ya sasa; na maeneo mapya yaongezwe ili sera iwe yenye kujitosheleza.

Baadhi ya maeneo ya sera yaliyokosa ufafanuzi wa kutosha ni pamoja na muundo wa elimu, ujuzi uliokusudiwa, lugha ya kufundishia, na umri wa kuanza elimu ya

awali na elimu ya msingi kutokuwa mahsusi. Eneo jingine la sera ambalo halikutekelezwa ni mfumo wa miaka kumi wa elimu ya lazima. Pia kulikuwa na kukosekana kwa muundo wa kutekeleza mahusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo; kutokuwepo kwa sheria ya elimumsingi na sekondari; kukosekana kwa utaratibu wa kuwaendeleza wanafunzi wenye vipaji, vipawa, na kasi tofauti na mahitaji maalum; na kukosekana kwa utaratibu na utambuzi wa maarifa, ujuzi, na stadi zilizopatikana nje ya mfumo rasmi wa shule. Maeneo mengine muhimu ambayo hayakuzingatiwa vema ni elimu ya ualimu, elimu ya juu, utafiti katika elimu na ushirikishwaji wa jamii katika utoaji wa elimu na mafunzo; na malengo ya jumla ya elimu kwa kila ngazi ya elimu na mafunzo.

Kwa kuzingatia muktadha huo, sera iliyopo imefanyiwa marekebisho na kutolewa kwa Rasimu ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la mwaka 2023.

## 2.2. Falsafa ya Elimu

Falsafa ya Elimu ya Kujitegemea itaendelea kuongoza utoaji wa elimu na mafunzo kwa kuzingatia mabadiliko yanayotokea kitaifa na kimataifa katika nyanja za siasa, jamii, uchumi, sayansi na teknolojia.

## 2.3. Madhumuni ya Jumla ya Elimu na Mafunzo

Yafuatayo ni madhumuni ya elimu na mafunzo nchini:

(a) Kukuza na kujenga haiba ya Mtanzania ili aweze kubadili maisha yake na kuchangia katika maendeleo ya jamii, Taifa na dunia;

(b) Kukuza uelewa na kuthamini utamaduni, mila na desturi za Watanzania, kuheshimu tofauti za kitamaduni, na kuwa na mitazamo chanya;

(c) Kumwezesha Mtanzania kukuza na kutumia kwa usahihi stadi za teknolojia, ubunifu, fikra tunduizi, uvumbuzi, ushirikiano na mawasiliano katika kujiletea maendeleo binafsi na ya taifa kwa ujumla;

(d) Kuendeleza na kukuza weledi, kujiamini, kudadisi, na heshima kwa utu na haki za binadamu na kuwa tayari kufanya kazi kwa kujiendeleza kibinafsi na maendeleo ya Taifa kwa ujumla;

(e) Kukuza na kupanua mawanda ya kujipatia maarifa, mtazamo chanya, uhodari, ujasiriamali, weledi na kuwezesha utamaduni unaothamini maendeleo ya binadamu ili kukidhi mahitaji halisi ya jamii;

(f) Kumwezesha Mtanzania kuelewa, kulinda na kuendeleza misingi ya maadili ya Taifa na uadilifu ikiwa ni pamoja na utu, uzalendo, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji, pamoja na kuthamini haki za kiraia, wajibu na majukumu yanayoendana na haki hizo;

(g) Kukuza utashi wa kupenda na kuheshimu kazi ili kuboresha utendaji kazi katika sekta mbalimbali ikiwemo teknolojia na ubunifu;

(h) Kukuza ushirikiano wa kitaifa, kikanda, na kimataifa, na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo Tanzania imeridhia;

(i) Kumwezesha Mtanzania kuelewa umuhimu wa kudumisha amani na haki kwa kuzingatia katiba ya nchi;

(j) Kuimarisha uwajibikaji wa pamoja katika kuboresha afya na ustawi wa watu na jamii, usawa wa kijinsia, usimamizi na utunzaji endelevu wa mazingira;

(k) Kukuza fursa za elimu isiyo na ukomo kwa watu wote kwa kuzingatia matendo jumuishi, haki, kujisimamia, kujali na kutoa afua stahiki kwa jamii; na

(l) Kuwezesha ujenzi wa ujuzi ili kuchochea mafanikio katika ulimwengu wa kazi na mafunzo ya kitaalamu.

## 2.4. Madhumuni ya Elimu na Mafunzo kwa Kila Ngazi ya Elimu

Madhumuni ya elimu na mafunzo nchini kwa kila ngazi ni kama ifuatavyo:

### 2.4.1. Elimu ya Awali

Elimu ya Awali inalenga kufikia malengo yafuatayo:

(a) Kumwandaa mtoto kimakuzi, kimwili, kiakili, kimaadili, kijamii na kijinsi;

(b) Kumwezesha mtoto kujitambua mwenyewe na mazingira yanayomzunguka;

(c) Kubaini mtoto mwenye mahitaji maalumu na kumpa fursa stahiki;

(d) Kumwezesha mtoto kumudu lugha mbalimbali; na

(e) Kumwandaa mtoto kujiunga na elimu ya msingi.

### 2.4.2. Elimu ya Msingi

Elimu ya Msingi inakusudia kufikia malengo yafuatayo:

(a) Kumwandaa mwanafunzi kuwa na stadi za kusoma, kuandika, na kuhesabu;

(b) Kumjengea mwanafunzi uwezo wa kuwasiliana kwa lugha fasaha, ikiwemo lugha ya Taifa ya Kiswahili, lugha za kigeni, Lugha ya Alama ya Tanzania (LAT), Lugha ya Alama Mguso na Breli;

(c) Kumjengea mwanafunzi misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria;

(d) Kumwezesha mwanafunzi kutambua, kuheshimu na kudumisha utamaduni wa Mtanzania na umoja wa kitaifa, na kutambua tamaduni nyingine;

(e) Kumjengea mwanafunzi ubunifu, uwezo wa kudadisi, kufikiri kiyakinifu na kutatua matatizo;

(f) Kukuza vipaji, vipawa, stadi za kazi, michezo na sanaa;

(g) Kumwezesha mwanafunzi kutambua na kutumia sayansi na teknolojia ya habari na mawasiliano katika kujifunza na kuendesha maisha ya kila siku;

(h) Kukuza maarifa, ujuzi na mwelekeo wa kutunza mazingira;

(i) kuheshimu usawa wa kijinsi;

(j) kumwezesha mwanafunzi kutambua masuala mtambuko; na

(k) Kumtayarisha mwanafunzi kuendelea na elimu ya sekondari.

### 2.4.3. Elimu ya Sekondari

Elimu ya sekondari inakusudia kufikia malengo yafuatayo:

(a) Kupanua, kuimarisha, na kuendeleza maarifa, stadi, na mtazamo chanya uliopatikana katika ngazi ya elimu ya msingi;

(b) Kumwezesha mwanafunzi kuelewa na kulinda misingi ya utamaduni (mila na desturi), umoja wa kitaifa, tunu za Taifa; na kuthamini haki za binadamu na wajibu unaoendana na haki hizo;

(c) Kujenga uelewa wa mwanafunzi kuhusu demokrasia, umuhimu na mipaka yake;

(d) Kujenga utamaduni na umahiri kwa mwanafunzi katika kujisomea, kujiamini, kujiendeleza kwenye nyanja za sayansi na teknolojia, maarifa ya kinadharia, kiufundi, kiujasiriamali na kupenda kufanya kazi;

(e) Kumwezesha mwanafunzi kutumia stadi za lugha mbalimbali;

(f) Kumwezesha mwanafunzi kutambua uwajibikaji wa pamoja wa kutunza afya, kuthamini usawa wa kijinsi na kusimamia utunzaji endelevu wa mazingira;

(g) Kuimarisha misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; na

(h) Kujenga ujuzi na stadi mbalimbali zitakazomwezesha mhitimu kujiunga na elimu ya juu na mafunzo ya amali sanifu baada ya elimu ya sekondari, kujiajiri, kuajiriwa, na kuyamudu maisha kwa kutumia mazingira yake.

### 2.4.4. Elimu ya Juu

Elimu ya Juu inalenga kufikia madhumuni yafuatayo:

(a) Kupanua, kuimarisha, na kuendeleza maarifa, stadi, na mtazamo chanya uliopatikana kabla ya kujiunga na elimu ya juu;

(b) Kumwezesha mwanafunzi kupata maarifa na stadi za juu za kitaaluma na kitaalamu;

(c) Kuandaa wanataaluma na wataalamu kwa ajili ya sekta mbalimbali;

(d) Kuimarisha misingi ya uadilifu na kuheshimu utawala wa sheria; na

(e) Kujenga uwezo wa wanataaluma na taasisi za elimu ya juu katika kutoa na kuendeleza maarifa mapya kupitia utafiti, machapisho yenye ubora na kutatua changamoto za kijamii.

## 2.5. Dira, Dhima na Malengo ya Sera

Msingi wa elimu na mafunzo utaendelea kujikita katika kumjengea Mtanzania misingi ya uzalendo, maadili, ujuzi, umahiri na kumwezesha kujitegemea kwa kuzingatia yafuatayo:

### 2.5.1. Dira

Kuwa na Mtanzania aliyeelimika, mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

### 2.5.2. Dhima

Kuinua ubora wa elimu na mafunzo kwa kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika, wenye stadi na wanaopenda kujiendeleza kielimu ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa.

### 2.5.3. Malengo ya Sera

Sera hii ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023, itakuwa na malengo ya jumla na mahususi kama ifuatavyo:

#### 2.5.3.1. Lengo la Jumla

Kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo unaoweza kumuandaa Mtanzania mwenye maarifa, stadi na mtazamo chanya utakaomwezesha kuchangia katika kuleta maendeleo endelevu ya Taifa.

#### 2.5.3.2. Malengo Mahsusi

Malengo mahsusi ya Sera ni:

(i) Kuwa na mfumo, muundo na utaratibu nyumbufu wa kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalam;

(ii) Kutoa fursa mbalimbali za elimu na mafunzo nchini;

(iii) Kuwa na elimu na mafunzo yenye viwango vya ubora unaotambulika kitaifa, kikanda na kimataifa;

(iv) Kuwa na rasilimali ya kutosha na yenye umahiri na weledistahiki kuendana na vipaumbelevya Taifa;

(v) Kuwa na usimamizi na uendeshaji madhubuti wa elimu na mafunzo nchini;

(vi) Kuwa na mfumo endelevu wa ugharimiaji wa elimu na mafunzo; na

(vii) Kuwa na mfumo wa elimu na mafunzo unaozingatia masuala mtambuka, ikiwemo elimu ya afya ya mazingira; magonjwa na majanga; utafiti na maendeleo ya sekta ya elimu; na ushirikiano wa sekta ya umma na binafsi katika utoaji wa elimu na mafunzo.

# SURA YA TATU

## MAENEO, MASUALA NA MATAMKO YA SERA

### 3.1. Mfumo, Miundo na Taratibu Nyumbufu

Sura hii inatoa ufafanuzi anuai kuhusu mfumo, miundo na taratibu nyumbufu zinazolenga kumwezesha kila Mtanzania kujiendeleza kwa njia mbalimbali kitaaluma na kitaalamu kama ilivyofafanuliwa katika sehemu zifuatazo:

#### 3.1.1. Mfumo na Muundo wa Elimu na Mafunzo

**Maelezo**

Serikali imewezesha upatikanaji wa fursa ya elimu kwa watoto wa jinsi zote. Kwa mfano, ripoti ya uandikishaji kwa shule za msingi inaonesha kuwa asilimia 108.5 ya wanafunzi waliandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2022. Hata hivyo, utaratibu wa kundelea na masomo baada ya elimu ya msingi umeendelea kuwa na changamoto kwa sababu mfumo uliopo sasa unachuja wanafunzi badala ya kutoa fursa ya kuwaendeleza kadiri ya uwezo, vipaji na vipawa vyao. Mfumo huu pia, kwa kiwango kikubwa umejikita katika taaluma pekee, hivyo kuwafanya wale wanaoshindwa kuendelea kitaaluma na kuchaguliwa kujiunga na elimu na mafunzo ya amali kuonekana kuwa wamefeli. Hiki ni kiashiria cha mfumo kutokuwa nyumbufu na hivyo kushindwa kutoa fursa anuai za elimu na mafunzo zinazoweza kumfanya kila mwanafunzi kupata ujuzi na maarifa kwa ajili ya ulimwengu wa kazi kulingana na uwezo, matakwa na malengo yake. Katika muktadha huo, mfumo nyumbufu wa elimu unahitajika.

Katika muundo wetu wa elimu wa $2+7+4+2+3^{+}$, mwanafunzi anayeanza masomo akiwa na umri wa miaka saba (7) atahitimu elimu ya juu akiwa na umri mkubwa, takribani miaka 25, ikilinganishwa na nchi kama Afrika Kusini, Mauritius, Malaysia na Finland, ambapo umri wa kijana anayemaliza elimu ya juu ni kati ya miaka 20 hadi 22. Kwa sababu hii, umri wa kuanza darasa la kwanza umepunguzwa kutoka miaka saba (7) hadi sita (6), kama ilivyo katika nchi nyingi duniani. Muundo huu utamwezesha mwanafunzi kukamilisha mzunguko wa masomo yake kwa muda mfupi zaidi.

### Lengo

Kujenga mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo wenye tija na ufanisi na hivyo kuongeza idadi ya wananchi walioelimika na mahiri katika fani mbalimbali kuendana na mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi.

### Matamko

*3.1.1.1 Serikali itaweka mfumo nyumbufu wa elimu na mafunzo ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kujielimisha na kuwa huru kutafuta elimu katika fani wanazopenda, kwa kutumia njia mbalimbali za kupata elimu na mafunzo ikiwemo huria na masafa kulingana na stahili na uwezo wao.*

*3.1.1.2 Mfumo wa elimu utajikita katika kujenga umahiri. Aidha, msisitizo utakuwa katika kupata ujuzi, maarifa, weledi, mwelekeo, mitazamo chanya, maadili mema na tabia zinazokubalika kulingana na mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi pamoja na kuzingatia Mfumo wa Tuzo wa Taifa.*

*3.1.1.3 Elimu katika mfumo rasmi itagawanyika katika ngazi za elimu ya awali, elimu ya msingi, elimu ya sekondari na elimu ya juu.*

*3.1.1.4 Muundo katika mfumo rasmi wa elimu na mafunzo utakuwa $1+6+4+2/3+3^{+}$, kwa maana ya mwaka mmoja wa elimu ya awali, miaka sita ya elimu ya msingi, miaka minne ya elimu ya sekondari kidato cha kwanza hadi cha nne, miaka miwili ya elimu ya sekondari kidato cha tano na sita au miaka mitatu ya amali sanifu, na miaka isiyopungua mitatu ya elimu ya juu.*

*3.1.1.5 Elimu ya lazima itajumuisha elimu ya msingi na elimu ya sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne na itatolewa kwa miaka 10.*

*3.1.1.6 Elimu ya msingi itakuwa elimu ya jumla kama itakavyofafanuliwa kupitia mitaala husika.*

*3.1.1.7 Elimu ya sekondari ya chini yaani kidato cha kwanza hadi cha nne,*

*itagawanyika katika mikondo miwili ambayo ni mkondo wa elimu ya jumla, na mkondo wa elimu ya amali.*

*3.1.1.8 Elimu ya amali itakuwa sehemu muhimu ya mfumo wa elimu na itatolewa kulingana na mitaala ya ngazi husika.*

*3.1.1.9 Elimu ya sekondari kidato cha tano na sita au elimu ya amali sanifu itakuwa hitaji la msingi kwa ajili ya kujiunga na elimu ya juu.*

*3.1.1.10 Elimu ya juu itakuwa elimu baada ya elimu ya sekondari na itagawanyika katika mkondo wa elimu ya jumla na elimu ya amali.*

*3.1.1.11 Serikali itaweka na kusimamia mfumo wa kitaifa wa ulinganifu wa sifa na tuzo katika ngazi zote.*

### 3.1.2. Elimu ya Lazima na Muda wa Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Muundo wa elimu na mafunzo uliopo sasa unatoa fursa ya mtoto kujiunga na elimu ya awali kwa muda wa miaka miwili. Hata hivyo, uchambuzi unaonesha kuwa mtaala unaotumika unaweza kufundishwa kwa mwaka mmoja kama ukifundishwa kwa ufanisi. Vilevile, watoto hupitia Vituo vya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto ambavyo huwaandaa kujiunga na elimu ya awali. Hata hivyo, kwa mujibu wa itifaki ya Dakar ya mwaka 2000 ambayo Tanzania imeiridhia na UNESCO ISCED (International Standard Classification of Education) ya mwaka 2011, elimu ya awali inatakiwa kutolewa kwa watoto wenye umri kati ya miaka mitatu hadi sita. Pamoja na kutambua umuhimu wa elimu katika ngazi hii, itifaki ya UNESCO inayataka mataifa kuhakikisha kuwa mtoto wa rika lengwa anapata elimu katika ngazi husika kulingana na mazingira ya kila nchi.

Kwa upande mwingine, mazingira ya elimu ya awali nchini hayaridhishi kwa sababu ya upungufu wa walimu wenye sifa na miundombinu stahiki. Kwa mfano, wastani wa uwiano wa mwalimu na mwanafunzi ulikuwa 1:94 kwa mwaka 2022, badala ya 1:25 unaotakiwa. Darasa la elimu ya awali kwa sasa lina wastani wa wanafunzi 80, zaidi ya mara tatu ya uwiano unaotakiwa.

Pia, kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Sura 353, elimu ya msingi ya sasa ni ya miaka saba (7) na ni ya lazima kwa uandikishaji na mahudhurio. Hivyo, wahitimu wengi wa elimu ya msingi katika mfumo wa sasa wanakuwa na umri wa miaka 13. Baadhi ya wahitimu huendelea na elimu ya sekondari na mafunzo ya ufundi na wanaokosa fursa hizo huingia kwenye ulimwengu wa kazi. Wahitimu hawa wanakuwa na umri mdogo na hawana maarifa na ujuzi unaotosheleza kujiunga na ulimwengu wa kazi au kukabiliana na changamoto za maisha pale wanapokosa fursa ya kuendelea na elimu ya sekondari au elimu ya ufundi.

Hata hivyo, mkataba wa kimataifa wa Shirika la Kazi Duniani umeweka umri wa chini wa kuajiriwa katika baadhi ya kazi kuwa miaka 15. Kadhalika, itifaki ya SADC (1997) kuhusu elimu na mafunzo inasisitiza kutokomeza changamoto ya kutojua kusoma na kuandika kwa kuweka juhudi ya kuwa na elimu ya lazima kwa wote kwa kipindi kisichopungua miaka tisa.

Hivyo basi, kutokana na changamoto za muundo uliopo wa $2+7+4+2+3^{+}$ na makubaliano hayo, Serikali kwa kushirikisha wadau wa elimu, imeona umuhimu wa kurekebisha muundo wa elimu ya awali ili itolewe kwa kipindi cha mwaka mmoja, elimu ya msingi kwa miaka sita na elimu ya sekondari chini kwa miaka minne. Elimu hii itakuwa ya lazima na itamwezesha mwanafunzi kumudu stadi za kusoma, kuandika na kuhesabu, kuwa na ufahamu wa jumla na pia kupata umahiri ikiwemo maarifa na ujuzi kulingana na matakwa ya ngazi hiyo.

### Lengo

Kuwa na muda wa utoaji wa elimu na mafunzo wenye kuleta tija, ufanisi na matumizi bora ya rasilimali.

### Matamko

*3.1.2.1 Serikali itaendelea kutambua elimu ya awali kuwa sehemu ya mfumo rasmi wa elimu na kuandaa utaratibu wa kuifanya kuwa ya lazima na kutolewa kwa watoto wenye umri wa miaka mitano kwa kipindi cha mwaka mmoja.*

*3.1.2.2 Elimu ya awali itajumuisha malezi na makuzi ya mtoto kwa lengo la*

*kumuandaa kimwili, kiakili, kihisia na kijamii ili kumwezesha kuishi na jamii na kujiunga na elimu ya msingi.*

*3.1.2.3 Serikali itaweka utaratibu wa elimu ya msingi na sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne kuwa ya lazima na kutolewa kwa miaka kumi. Pia, umri wa kuanza darasa la kwanza utakuwa miaka sita.*

*3.1.2.4 Serikali itahakikisha kuwa elimu ya awali, msingi na sekondari inatolewa bila ada katika mfumo wa umma.*

## 3.2. Fursa Mbalimbali za Elimu na Mafunzo

### 3.2.1. Fursa za Usawa katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Ni muhimu kwa kila Mtanzania kupata fursa sawa za elimu na mafunzo bila ubaguzi wa jinsi, rangi, kabila, dini, ulemavu, hali ya kijamii au kipato. Ushiriki wa jinsi zote katika elimu na mafunzo ni muhimu katika kuhakikisha kuwa kila Mtanzania anashiriki kikamilifu katika kuchangia maendeleo ya Taifa. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kutoa elimu na mafunzo kwa kuzingatia usawa kwa makundi yote bila kumuacha yeyote nyuma. Vilevile, Serikali, kwa kushirikiana na wadau wa elimu, imeendelea kupanua na kuboresha mazingira ya utoaji elimu jumuishi na kumwezesha kila Mtanzania kupata fursa za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji yake, mazingira na hali halisi ya upatikanaji rasilimali nchini.

Pamoja na juhudi hizo za Serikali na wadau wengine, bado baadhi ya makundi hayajafikiwa kikamilifu kutokana na sababu za kijamii, kiafya, kiuchumi na kijiografia, hasa umbali wa kutembea kwenda na kutoka shuleni, ajira za watoto, utoro, umaskini, mimba na ndoa za utotoni. Ingawa uwiano wa kijinsi katika ngazi ya elimu ya msingi na sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne unaridhisha, ushiriki wa wasichana katika elimu ya juu, hususan katika fani za sayansi, hisabati na teknolojia bado hauridhishi kwani ni asilimia 37.5 tu ya wasichana waliojiunga na fani hizo kwa mwaka 2022.

Kwa sababu hizo, ili kufikia lengo la kutoa elimu kwa wote, kuna umuhimu wa

kuondoa vikwazo vyote vinavyosababisha baadhi ya wanafunzi kushindwa kujiunga na kukamilisha mzunguko wa elimu na mafunzo. Pia, Serikali imenuia kuweka mazingira wezeshi ili kuimarisha uwiano wa kijinsi katika elimu ya amali na elimu ya juu, hususan katika fani za sayansi, hisabati na teknolojia.

### Lengo

Kuhakikisha kuwa watoto wa jinsi zote na rika lengwa wanajiunga na kukamilisha mzunguko wa elimu na mafunzo katika ngazi husika.

### Matamko

*3.2.1.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuongeza na kuimarisha fursa anuai za elimu na mafunzo kwa makundi yote ya kijamii.*

*3.2.1.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mazingira wezeshi ya kuongeza ushiriki wa wasichana na wavulana katika elimu ya amali na elimu ya juu hususan katika fani za sayansi, hisabati, na teknolojia.*

*3.2.1.3. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaondoa vikwazo vinavyozuia wanafunzi wote kuanza, kuendelea na kukamilisha mzunguko wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.2.1.4. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha na kusimamia afua mbalimbali zinazolenga kutoa fursa za elimu na mafunzo kwa wale walioikosa.*

## 3.2.2. Elimu na Mafunzo Jumuishi Ngazi Zote

### Maelezo

Lengo la nne la Malengo ya Maendeleo Endelevu linahimiza uwepo wa mfumo jumuishi unaompa kila mtoto haki ya kupata elimu. Katika mfumo huo, wanafunzi wote wakiwemo wenye mahitaji maalumu, hujifunza pamoja kulingana na umri wao katika shule zilizopo katika jamii yao. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuboresha mazingira ya kuwajumuisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu kushiriki kikamilifu katika mfumo rasmi wa elimu.

Hata hivyo, zipo changamoto kadhaa zinazoathiri utoaji wa elimu jumuishi ikiwemo ukosefu wa mfumo fanisi wa utambuzi wa watoto wenye mahitaji maalumu, uhaba mkubwa wa walimu mahiri wa elimu maalumu, uhaba wa vifaa saidizi na mtizamo hasi wa jamii kwa watoto wenye mahitaji maalumu. Hivyo, ni muhimu kuendelea kuboresha mfumo wa utoaji wa elimu na mafunzo katika mazingira jumuishi ili kutoa fursa kwa watoto wote kujifunza kwa kushirikiana.

### Lengo

Kuimarisha utoaji wa elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote.

### Matamko

*3.2.2.1. Serikali itaimarisha mfumo wa utambuzi wa mahitaji maalumu ya kila mwanafunzi katika ngazi zote za elimu.*

*3.2.2.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa mazingira wezeshi ya utoaji wa elimu na mafunzo jumuishi katika ngazi zote.*

## 3.2.3. Utambuzi na Uendelezaji wa Vipaji na Vipawa

### Maelezo

Ili kufikia lengo la maendeleo ya Taifa, ni muhimu kutambua mapema na kuendeleza vipawa na vipaji katika fani mbalimbali kama vile sayansi na teknolojia, muziki, ngoma, sanaa, ufundi na michezo. Hata hivyo, utaratibu uliopo sasa unazingatia ufaulu wa kitaaluma kama kigezo pekee cha kutambua vipaji na vipawa na hivyo kuwapoteza wanafunzi wengi wenye vipaji na vipawa katika maeneo mengine. Kwa sababu hiyo, Serikali imeona umuhimu wa kutengeneza utaratibu utakaotambua wenye vipaji na vipawa kwa upana zaidi badala ya kigezo kimoja tu cha ufaulu wa kitaaluma katika mitihani.

Hatua hii ni muimu kwa sababu uendelezaji wa vipaji na vipawa unachangia katika kujenga Taifa kwa namna tofauti tofauti. Kwa mfano, vipaji katika michezo vinachangia katika kuimarisha nidhamu na mahusiano, maelewano na mshikamano; vipaji hivyo hukuza ukakamavu, ujasiri na kujiamini; vinalitambulisha Taifa nje ya mipaka na pia kumjenga mwanafunzi kuwa timamu kimwili, kiakili na

kiroho. Kwa muktadha huo, kuna umuhimu wa Serikali kuendelea kutoa msukumo na kuimarisha mfumo wa kubaini na kuendeleza vipaji na vipawa katika nyanja mbalimbali nchini.

### Lengo

Kuimarisha mfumo wa kubaini na kuendeleza vipaji na vipawa mbalimbali katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.2.3.1. Serikali itaweka utaratibu wa kubaini na kuendeleza wanafunzi wenye vipaji na vipawa mbalimbali katika ngazi zote za elimu.*

*3.2.3.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha elimu kwa michezo katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

## 3.3. Matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

### Maelezo

TEHAMA ni nyenzo muhimu katika ulimwengu wa sasa wa kazi. Maendeleo ya teknolojia, hususan TEHAMA, yametoa fursa ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa kutumia njia anuai zikiwemo za masafa na huria. Hali hii inamwezesha mwalimu mmoja kuweza kufikia makundi mbalimbali ya wanafunzi kwa wakati mmoja. Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ya Mwaka 2016 ilihamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji wa elimu na mafunzo kupitia mfumo rasmi na nje ya mfumo rasmi. Kwa sababu hizo, katika mazingira yenye uhaba wa walimu, wakufunzi na wahadhiri wa baadhi ya masomo kama vile lugha, hisabati na sayansi, njia hii inaweza kutumika kwa ufanisi kutoa elimu bora kwa wanafunzi wengi zaidi kwa kutumia idadi ndogo ya walimu mahiri. Hili linaweza kufanikiwa ikiwa tu miundombinu na vifaa vya TEHAMA kwa wanafunzi vinapatikana na kuongezeka.

Pamoja na hayo yote, bado Tanzania ni moja ya nchi zenye changamoto ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji. Hali hii inatokana na upungufu wa vifaa na rasilimaliwatu katika ufundishaji wa TEHAMA. Upungufu huo

unasababisha wahitimu kukosa umahiri stahiki wa kuchagiza maendeleo ya sayansi na teknolojia na kuiwezesha nchi kujenga uchumi shindani katika dunia ya utandawazi. Ukweli ni kwamba, endapo TEHAMA itafundishwa kwa ufanisi, itazalisha rasilimaliwatu yenye ujuzi stahiki kwa maendeleo ya Taifa. Aidha, kuimarisha ufundishaji wa TEHAMA ni moja ya nyenzo muhimu ya kukuza ubunifu na uwezo wa kutatua matatizo. Hivyo, kuna umuhimu mkubwa wa kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

#### Lengo

Kuimarisha matumizi ya teknolojia ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo.

#### Matamko

*3.3.1.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inatumika katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote kulingana na mahitaji.*

*3.3.1.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mazingira wezeshi ya utoaji wa elimu na mafunzo kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika ngazi zote.*

### 3.4. Utambuzi wa Watu Waliopata Ujuzi na Maarifa Nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Elimu na mafunzo nje ya mfumo rasmi ni njia mojawapo ya kujenga umahiri katika fani na stadi mbalimbali duniani kote. Serikali imekwisha kuweka utaratibu wa kutambua na kurasimisha ujuzi unaopatikana nje ya mfumo rasmi katika fani mbalimbali za amali kwa lengo la kuwawezesha walengwa kushiriki kikamilifu katika ulimwengu wa kazi. Licha ya jitihada hizo, utaratibu unaotumika sasa umejikita zaidi kwenye fani chache za kihandisi na kuacha fani nyingine. Hivyo, kuna kila sababu ya kuongeza wigo wa utaratibu huo ili uweze kujumuisha fani zote muhimu za amali.

### Lengo

Kuwa na mfumo wa kutambua na kurasimisha ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.4.1.1. Serikali itaimarisha utaratibu wa utambuzi na urasimishaji wa maarifa, ujuzi na stadi zinazopatikana nje ya mfumo rasmi wa elimu na mafunzo.*

*3.4.1.2. Elimu nje ya mfumo rasmi itatambuliwa, na watakaopitia mfumo huo watakuwa na fursa ya kujiunga na mfumo rasmi wa elimu kulingana na vigezo vitakavyowekwa.*

## 3.5. Elimu ya Watu Wazima na Endelevu

### Maelezo

Ni muhimu kwa kila Mtanzania kupata fursa ya kujiendeleza kielimu kulingana na uwezo na mahitaji yake binafsi, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia bila ubaguzi wa umri na jinsi.

Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imeendelea kuongeza fursa na kuboresha mazingira ya utoaji Elimu ya Watu Wazima na Endelevu ili kila Mtanzania apate haki ya kujiendeleza kwa kuzingatia mahitaji yake. Pamoja na jitihada za Serikali na wadau, bado kasi ya kupungua kwa idadi ya watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu ni ndogo.

Kwa sababu hiyo, kuna uhitaji mkubwa wa elimu endelevu kutokana na mabadiliko ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Hivyo, ni muhimu kuimarisha fursa za upatikanaji wa elimu ya watu wazima na endelevu.

### Lengo

Kuimarisha mfumo wa elimu ya watu wazima na endelevu.

### Matamko

*3.5.1.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka utaratibu na mazingira wezeshi ya kuhakikisha kuwa elimu ya watu wazima na endelevu*

*inatolewa kwa ufanisi katika ngazi zote kwa njia mbalimbali ikiwemo huria na masafa.*

3.5.1.2. *Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuhamasisha jamii ya Watanzania kuwa na ari ya kujiendeleza kielimu kwa njia mbalimbali ikiwemo huria na masafa.*

## 3.6. Ubora wa Elimu na Mafunzo

Mfumo huu mpya wa elimu unalenga kutoa elimu na mafunzo yanayotambulika kikanda na kimataifa na yanayokidhi mahitaji ya maendeleo ya Taifa. Hoja hii imejikita katika masuala yafuatayo:

### 3.6.1. Mitaala ya Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Mtaala ni mwongozo wa elimu katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Ikiwa mtaala hautaandaliwa vizuri, kutekelezwa ipasavyo au kutathminiwa kwa umakini, mfumo wa elimu utakosa tija na hautaweza kuleta matarajio yanayokusudiwa katika jamii. Hadi kufikia mwaka 2005, mitaala ya elimu ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu ilijikita zaidi katika maudhui ya ufahamu huku ikiwa na msisitizo mdogo katika kujenga ujuzi. Kuanzia mwaka huo wa 2005, mitaala hiyo iliboreshwa na kuwa ya kujenga umahiri, kwa kuingiza stadi za kuajirika kutokana na mfumo wa kutoa mafunzo kwa nadharia na vitendo. Mitaala hii ilitekelezwa kwa kushirikiana na viwanda, mashamba na taasisi za huduma ili kuunganisha utoaji wa mafunzo kwa nadharia na vitendo. Hata hivyo, hapakuwa na maandalizi ya kutosha ya utekelezaji wa mitaala hiyo; mathalan, maandalizi ya walimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia havikukidhi mahitaji. Sasa, kuna umuhimu wa kuimarisha mitaala katika ngazi zote pamoja na kuhakikisha kwamba walimu wanatayarishwa vyema kumudu utekelezaji wa mitaala yenye kujenga umahiri.

Kwa upande mwingine, uzoefu unaonesha kuwa baadhi ya mitaala ya amali na elimu ya juu haiwaandai ipasavyo wahitimu wake kwa ajili ya ulimwengu wa kazi. Hivyo, kuna umuhimu wa kupitia upya mitaala ya elimu ya amali na elimu ya juu ili

ikidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi. Pia, tathmini zinaonesha uwepo wa tofauti kubwa ya maudhui katika baadhi ya programu za elimu ya juu ambazo kimsingi zingetakiwa kufanana. Kwa mantiki hiyo, kuna umuhimu wa kuweka vigezo vya ulinganifu baina ya programu zinazofanana katika taasisi mbalimbali. Pia kuna umuhimu wa mitaala ya ngazi zote kuzingatia stadi za msingi za karne ya 21 kama vile kuwasiliana, kushirikiana, ubunifu, fikra tunduizi, utatuzi wa matatizo, ujuzi wa kidijitali, ujasiriamali, maadili na uzalendo.

Zaidi ya hayo, utandawazi, tofauti za kiuchumi na muingiliano wa watu wenye tamaduni mbalimbali umechangia katika kuleta mabadiliko ya maadili na tabia na hivyo kuleta changamoto mbalimbali katika jamii. Elimu ndiyo mhimili wa Taifa kudumisha amani na maadili yanayokubalika na jamii kwa kujenga stadi za kutatua migogoro, kujenga umoja wa kijamii na mshikamano. Kwa mantiki hiyo, kuna umuhimu wa kuwa na elimu inayolenga kuwasaidia wanafunzi kujenga uwezo wa kuzuia na kutatua migogoro kwa amani inapotokea miongoni mwa watu na baina ya makundi, kitaifa au kimataifa. Hivyo, mitaala ya elimu na mafunzo inapaswa kumwezesha Mtanzania kuelewa, kulinda na kuendeleza misingi ya amani, maadili ya Taifa na uadilifu, yaani utu, uzalendo, umoja, uwazi, uaminifu, uwajibikaji, pamoja na kuthamini haki za kiraia, wajibu na majukumu yake.

### Lengo

Kuboresha mitaala ya elimu na mafunzo ili kukidhi mahitaji ya ulimwengu wa kazi na kuhimili ushindani.

### Matamko

*3.6.1.1. Serikali itahakikisha uwepo wa mitaala bora katika ngazi zote za elimu na mafunzo inayoendana na wakati na inayozingatia mahitaji ya Taifa na ulimwengu wa kazi.*

*3.6.1.2. Serikali itahakikisha inawaandaa walimu, wakufunzi na wahadhiri kutekeleza kwa ufanisi mitaala inayojenga umahiri na kukuza stadi za karne ya 21 kwa wanafunzi.*

3.6.1.3. *Serikali itahakikisha kuwa mafunzo ya ualimu yanakuwa na mwendelezo wa kitaaluma na kitaalamu kati ya ngazi moja na nyingine na kuwepo kwa muda wa mafunzo chini ya uangalizi.*

3.6.1.4. *Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utoaji wa elimu ili kuwawezesha wahitimu wa ngazi zote kupata maarifa, ujuzi, umahiri na stadi za ujasiriamali ili kuchangia kikamilifu katika maendeleo ya taifa.*

3.6.1.5. *Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utaratibu wa utoaji wa elimu na mafunzo kwa nadharia na vitendo katika ngazi zote kwa ushirikiano na viwanda, mashamba na sekta nyingine za uzalishaji na utoaji huduma.*

3.6.1.6. *Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa utekelezaji wa mitaala unaakisi mahitaji ya ujuzi kulingana na mazingira na rasilimali zilizopo katika maeneo husika.*

3.6.1.7. *Serikali itaimarisha usimamizi na upimaji wa utekelezaji wa mitaala katika taasisi za elimu na mafunzo katika ngazi zote, ili kuleta ufanisi wa elimu na mafunzo yatolewayo.*

3.6.1.8. *Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha masuala ya ukatili wa kijinsia, stadi za kudumisha amani, uzalendo, maadili na utawala bora zinajumuishwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

3.6.1.9. *Serikali itaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Historia ya Tanzania na Maadili inafundishwa katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

### 3.6.2. Uthibiti Ubora wa Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Ubora wa elimu na mafunzo unatokana na ubora wa mitaala iliyopo, umahiri wa watekelezaji wa mitaala hiyo, uongozi, usimamizi, mazingira ya kutolea elimu na mafunzo, tathmini na rasilimali zilizopo. Licha ya maboresho mbalimbali

yaliyofanyika, bado kuna changamoto katika suala la ubora wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.

Kwa mfano, pamoja na ufaulu katika mitihani ya darasa la saba na kidato cha nne kuongezeka kutoka asilimia 57 mwaka 2014 hadi kufikia asilimia 79.7 mwaka 2022 kwa upande wa elimu ya msingi; na asilimia 69.8 mwaka 2014 hadi asilimia 87.8 mwaka 2022 kwa elimu ya sekondari ya chini (kidato cha 1 – 4), bado kiwango cha maarifa na ujuzi wa wahitimu katika ngazi hizo ni kidogo ikilinganishwa na ngazi ya elimu waliyofikia. Kadhalika, maarifa na ujuzi wa wahitimu wa mafunzo ya ufundi na elimu ya juu hayakidhi mahitaji mbalimbali katika ulimwengu wa kazi.

Aidha, kwa mujibu wa tathmini zilizofanyika, mitaala bora na uthibiti fanisi wa elimu; uimarishaji wa upimaji na tathmini, ithibati na mamlaka zinazohusika na masuala hayo ni muhimu sana katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo nchini.

Kwa upande wake, wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo imekuwa ikifanya juhudi za kufuatilia ubora wa elimu katika ngazi zote kwa kuzingatia mitaala na viwango vilivyowekwa. Hata hivyo, uthibiti ubora wa elimu ya awali, elimu ya msingi, sekondari na elimu ya ualimu unaoratibiwa na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, umekuwa ukikabiliwa na changamoto mbalimbali na hivyo kushindwa kufikia matarajio. Aidha, pamoja na kutumika kwa dhana ya uthibiti ubora wa shule yenye kuhitaji ushirikishwaji wa wadau na mbinu mbadala, changamoto ya dhana ya ukaguzi wa shule yenye kujikita katika uhakiki wa orodha ya masuala yanayohitajika kufanyika katika ufundishaji na ujifunzaji imetawala. Hivyo, kuna uhitaji wa kuimarisha utekelezaji wa dhana ya uthibiti ubora inayozingatia ushirikishwaji na uwajibikaji wa pamoja wa kamati na bodi za shule na vyuo, wakuu wa vyuo vya ualimu, walimu wakuu, wakuu wa shule, walimu, wakufunzi pamoja na wazazi katika suala la usimamizi na uthibiti ubora wa elimu itolewayo nchini.

Kwa upande mwingine, wizara imekasimu jukumu la kuratibu ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi (amali) kwa NACTVET. Pia, wizara imekasimu jukumu la kuratibu ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya juu ya jumla kwa TCU. Vyombo hivi vya ithibati vinashirikiana na taasisi nyingine wezeshi ikiwa ni pamoja na Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), NECTA, Bodi ya Huduma za

Maktaba Tanzania (BOHUMATA), Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW) na Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) katika kuinua ubora wa elimu. Hata hivyo, kumekuwa na changamoto za kiutendaji na za kiuratibu zinazoathiri viwango vya ubora wa elimu katika ngazi mbalimbali.

Hivyo, uhusiano baina ya taasisi zenye jukumu la kuwezesha na kusimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini na Wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo unahitaji kufanyiwa tathmini ya mara kwa mara kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika kwa lengo la kuongeza tija. Pia, sheria za taasisi hizo zinahitaji kutathminiwa ili kuleta muunganiko katika mfumo wa ithibati, uthibiti, usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo nchini.

### Lengo

Kuimarisha uratibu, usimamizi, ithibati na uthibiti katika utoaji wa elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.6.2.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha mfumo, muundo na taratibu za usimamizi, ithibati na uthibiti ubora wa malezi, elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.6.2.2. Serikali itaimarisha ithibati na uthibiti ubora wa elimu ya ualimu kwa kuweka utaratibu unaojumuisha ngazi mbalimbali za taaluma ya ualimu.*

*3.6.2.3. Serikali itahakikisha kuwa vyombo vya usimamizi, uendeshaji na uwezeshi katika utoaji wa elimu na mafunzo vinahusiana na kushirikiana katika ngazi zote.*

*3.6.2.4. Serikali itaimarisha mfumo, mbinu, dhana, na falsafa ya uthibiti ubora wa elimu na mafunzo ili kuleta ufanisi wa utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

## 3.6.3. Elimu ya Sayansi na Teknolojia

### Maelezo

Elimu ya sayansi na teknolojia ni muhimu katika kumwezesha mwananchi kumudu mazingira yake na kuchangia katika maendeleo ya Taifa. Kwa mantiki hiyo,

wanafunzi wa elimu ya msingi huanza kufundishwa somo la sayansi wakiwa darasa la III. Kwa upande wa elimu ya Sekondari Kidato cha 1 - 4, wanafunzi wote husoma masomo ya sayansi yaani Fizikia, Kemia, Baiolojia na Hisabati hadi kidato cha pili (II). Aidha, wanafunzi wote huendelea kusoma Baiolojia na Hisabati hadi kidato cha nne (IV) yakiwa ni masomo ya lazima, huku Fizikia na Kemia yakiwa masomo ya hiari katika kidato cha 3 na cha 4 ambapo wanafunzi wengine huchagua kuendelea na masomo hayo. Takwimu zinaonesha kuwa ni asilimia kati ya 30 na 35 tu ya wanafunzi husoma masomo ya sayansi katika kidato cha tatu (3) na cha nne (4). Wanafunzi hawa wakifaulu mitihani ya masomo hayo kidato cha nne, hutarajiwa kusomea tahasusi na fani za sayansi na teknolojia katika ngazi ya sekondari kidato cha tano (5) na sita (6), vyuo vya elimu ya juu na vyuo vya elimu ya ufundi sanifu na mafunzo ya ufundi stadi.

Idadi hii ndogo ya wanafunzi inatoa picha kwamba mitaala ya elimu ya msingi na sekondari inatakiwa kuweka mkazo katika elimu ya sayansi na teknolojia. Hii inapatana na Makubaliano kuhusu Elimu ya Sayansi na Teknolojia (UNESCO-Perth 2007) kwani yanasisitiza kufanya mapitio ya mitaala ya elimu ya sayansi na teknolojia ili kuongeza hamasa ya wanafunzi kutambua umuhimu wa sayansi na teknolojia katika jamii. Hii ndiyo sababu Serikali imeona kuwa kuna umuhimu wa kuendelea kuweka mkazo na kuchagiza matumizi ya sayansi na teknolojia katika kufundisha na kujifunza.

### Lengo

Kuongeza wigo wa wananchi walioelimika katika sayansi na teknolojia na wanaomudu kuitumia katika kuboresha maisha yao ya kila siku.

### Matamko

*3.6.3.1. Serikali itaimarisha muundo na utaratibu wa ufundishaji wa masomo ya Hisabati, Sayansi na Teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.6.3.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuhamasisha na kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Hisabati, Sayansi na Teknolojia katika ngazi zote za elimu na mafunzo na katika jamii.*

### 3.6.4. Nyenzo, Vifaa na Zana za Kufundishia na Kujifunzia

#### Maelezo

Utekelezaji wenye ufanisi wa mitaala unategemea upatikanaji wa nyenzo, vifaa na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia kulingana na mahitaji ya masomo na programu katika ngazi mbalimbali za elimu. Nyenzo, vifaa, na zana hizo ni pamoja na vitabu vya kiada na ziada, kemikali za maabara, mitambo na karakana. Utekelezaji wa elimu bila ada umekuwa na matokeo chanya yaliyoleta ongezeko la wanafunzi katika taasisi za elimu na mafunzo nchini na hivyo kusababisha upungufu wa jumla wa nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote za elimu.

Kwa mfano, mwaka 2022 idadi ya wanafunzi kwa elimu ya msingi ilikuwa 11,420,937 na sekondari 2,823,588. Pia, kulikuwa na kompyuta za mezani na mpakato 10,165 ikiwa ni sawa na uwiano wa 1:1,123 kwa shule za msingi na 42,377 sawa na uwiano wa 1:67 yaani kompyuta moja kwa wanafunzi 67 kwa shule za sekondari. Vilevile, kuna changamoto katika mfumo wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vitabu na uandaaji wa zana na nyenzo nyingine kwani haukidhi mahitaji. Aidha, baadhi ya vifaa, zana na nyenzo zilizopo, ama zimepitwa na wakati au haziendani na mahitaji ya sasa. Hali hii imekuwa ikichangia kudhoofisha utoaji wa elimu na mafunzo yenye ubora unaotakiwa.

Katika hali hii, kuna kila sababu ya kuanzisha na kuendelea kuboresha utaratibu wa upatikanaji wa vitabu, nyenzo, vifaa na zana bora za kutosha kukidhi mahitaji. Vilevile, ni muhimu kuwa na mfumo wenye tija wa uandaaji, uchapishaji na usambazaji wa vifaa vyote vya kufundishia na kujifunzia. Aidha, ni hitaji la msingi kutenga rasilimali fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya wanafunzi kulingana na viwango vilivyowekwa. Kuna umuhimu pia wa kuhamasisha utamaduni wa kujisomea na kuimarisha huduma za maktaba na njia mbadala za upatikanaji wa maarifa.

#### Lengo

Kuimarisha nyenzo, vifaa na zana za kufundishia na kujifunzia.

### Matamko

*3.6.4.1. Serikali itahakikisha uwepo wa nyenzo, vifaa na zana stahiki za kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

*3.6.4.2. Serikali itatoa na kusimamia matumizi ya kitabu kimoja cha kiada kwa kila somo kwa kila mwanafunzi katika elimu ya msingi na sekondari.*

*3.6.4.3. Serikali itahakikisha uwepo wa mfumo wenye tija wa uandaaji na usambazaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia katika ngazi zote za elimu.*

*3.6.4.4. Serikali itasimamia upatikanaji na matumizi ya vitabu vya ziada na rejea kwa kila somo katika elimu ya msingi na sekondari ambavyo vitaidhinishwa kwa utaratibu maalumu.*

*3.6.4.5. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa rasilimali fedha za kutosha kukidhi mahitaji ya vifaa vya kufundishia na kujifunzia kulingana na viwango vilivyowekwa katika ngazi zote za elimu.*

*3.6.4.6. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa wa huduma bora za maktaba na njia mbadala za upatikanaji wa maarifa katika shule, vyuo na jamii ili kuhamasisha utamaduni wa kujisomea.*

## 3.7. Miundombinu katika Taasisi za Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Kwa kiasi kikubwa, ufanisi katika utoaji wa elimu unategemea uwepo wa miundombinu bora. Katika miaka ya hivi karibuni, Serikali imeongeza miundombinu pamoja na samani katika taasisi zote za elimu. Pamoja na jitihada hizo, bado kuna changamoto kadhaa za miundombinu na hivyo Serikali kuona umuhimu wa kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu rafiki na ununuzi wa samani katika taasisi za elimu na mafunzo ili kufikia viwango vya ubora stahiki. Kwa mfano, takwimu za mwaka 2022 zinaonesha kuwa wastani wa uwiano wa darasa kwa wananfunzi katika elimu ya msingi ilikuwa 1:70 ukilinganisha na uwiano stahiki wa

1:45; na kwa upande wa elimu ya sekondari uwiano ulikuwa 1:36 ukilinganisha na uwiano stahiki wa 1:35 na bado Serikali inakusudia kuanzisha mkondo wa elimu ya amali katika ngazi ya sekondari kidato cha kwanza mpaka cha nne. Tathmini inaonesha kuwa zipo shule za sekondari 9 ambazo zitahitaji kufanyiwa ukarabati mkubwa na kuongezewa uwezo wa kudahili wanafunzi wengi ili kuziwezesha kuanza kutoa elimu ya amali. Shule hizo ni chache ukilinganisha na lengo la kuwa na asilimia 30 ya shule zote za Sekondari Kidato cha 1 - 4 zinazotegemewa kutoa mafunzo ya amali nchini. Hii inamaanisha kuwa uwekezaji katika miundombinu ya madarasa na karakana katika ngazi hii ya elimu kwa ajili ya mafunzo ya amali ni muhimu sana.

Zaidi ya hayo, Serikali, jamii na wadau wanahitaji kujenga utamaduni wa kutunza na kuhifadhi, kukarabati na kukarafati miundombinu ya taasisi za elimu na mafunzo.

### Lengo

Kuwa na miundombinu na samani toshelevu katika taasisi zote za elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.7.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha uwepo wa miundombinu, vifaa na samani bora, toshelevu na rafiki katika taasisi za elimu na mafunzo.*

*3.7.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha inaweka utaratibu mzuri wa utunzaji na ukarabati wa miundombinu, vifaa na samani katika taasisi za elimu na mafunzo.*

## 3.8. Mazingira Salama, Rafiki na Huduma Muhimu Katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Mazingira salama na rafiki pamoja na huduma bora ni mahitaji muhimu na ya msingi katika kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa kuna mazingira salama na rafiki katika

taasisi za elimu. Mathalani, Serikali imehakikisha uwepo wa huduma muhimu za kijamii kama vile chakula na lishe, maji safi na salama, vituo vya afya, umeme, mawasiliano na usafiri katika taasisi za elimu. Hata hivyo, bado kuna baadhi ya taasisi ambazo zinakabiliwa na mazingira yasiyoridhisha ya kihuduma kwa utoaji wa elimu stahiki.

Kwa upande mwingine, miaka ya hivi karibuni kumekuwa na ongezeko la vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia na ukatili kwa watoto. Vitendo hivyo ni pamoja na ubakaji, ulawiti, vipigo, adhabu kali, na utumikishwaji wa wanafunzi shuleni. Vitendo hivyo vimekuwa na madhara makubwa kwa watoto kimwili, kiakili, kisaikolojia na hata kusababisha mimba za utotoni na wanafunzi kuacha shule. Hivyo, kuna umuhimu wa kuendelea kuboresha mazingira pamoja na kuhakikisha uwepo wa huduma zinazokidhi mahitaji muhimu ya utoaji bora wa elimu na mafunzo katika taasisi zote za elimu nchini.

Ili kuleta tija katika ufundishaji na ujifunzaji, afya ya akili na mtizamo chanya ni mahitaji ya msingi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuwezesha upatikanaji wa huduma za ushauri na unasihi ili kuimarisha afya ya akili na mtizamo chanya kwa walimu na wanafunzi kwa lengo la kujenga mwelekeo, tabia na kuendeleza mila, desturi na maadili mema katika jamii. Pamoja na jitihada hizo za Serikali, bado kuna changamoto ya uchache wa wataalam na hivyo kupunguza ufanisi katika utoaji wa huduma hizo katika taasisi za elimu na mafunzo, hususan katika shule za msingi na sekondari. Hali hii inachangia mmomonyoko wa maadili ambao huleta athari kadhaa kama vile mimba za utotoni, utoro na utovu wa nidhamu. Hali hii pia husababisha msongo wa mawazo na sonona, na uchaguzi wa masomo usio sahihi kwa wanafunzi. Hivyo, ni muhimu kuimarisha utoaji wa huduma za ushauri na unasihi kwa wanafunzi na wafanyakazi katika taasisi zote za elimu na mafunzo.

### Lengo

Kutengeneza mazingira salama na rafiki, na kuhakikisha uwepo wa huduma muhimu katika taasisi za elimu na mafunzo.

**Matamko**

*3.8.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa inajenga mazingira salama na rafiki katika upatikanaji wa elimu na mafunzo.*

*3.8.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa huduma muhimu zikiwemo chakula na lishe, mawasiliano, umeme, maji safi na salama na afya zinapatikana katika taasisi za elimu na mafunzo.*

*3.8.3. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utoaji wa huduma stahiki ya ushauri na unasihi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

## 3.9. Matumizi ya Lugha katika Mawasiliano

### Maelezo

Ubora wa elimu na mafunzo kwa kiasi kikubwa unategemea ujuzi wa walimu na wanafunzi katika kuielewa na kuitumia lugha inayotumika katika kufundishia, kujifunzia na kuwasiliana. Kwa sasa, lugha za Kiswahili na Kiingereza, na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kama masomo katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Aidha, LAT, Lugha ya Alama Mguso na maandishi ya Breli ni masomo yanayofundishwa katika vyuo vya ualimu.

Kwa upande mwingine, lugha ya Kiswahili ni lugha ya Taifa na inatumika kama lugha ya kwanza au ya pili miongoni mwa wananchi wengi. Kiswahili pia kimekua kwa kiwango cha kimataifa hivyo kinatumiwa na wengi kupata maarifa na ujuzi katika nyanja na ngazi mbalimbali za elimu. Aidha, Tanzania imeridhia itifaki ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika kuhusiana na maendeleo na matumizi ya Kiswahili, ambapo Tanzania imechaguliwa kuwa makao makuu ya Taasisi ya Kuendeleza Kiswahili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Wakati huo huo, lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha ya pili au ya tatu kwa baadhi ya wananchi. Kwa muktadha huu, Kiswahili na Kiingereza ni lugha rasmi za kiofisi. Hivyo basi, ufahamu mzuri wa lugha ya Kiingereza na lugha nyingine za kigeni unamwezesha Mtanzania kuwasiliana na watu wa mataifa mengine na

kupata elimu, ujuzi na maarifa. Aidha, LAT, Lugha ya Alama Mguso, na maandishi ya Breli hutumika kwa mawasiliano baina ya viziwi, wasioona, viziwi wasioona, wale wenye uoni hafifu na watu wengine.

Kwa kutambua umuhimu huo wa lugha, Serikali imeendelea kusimamia na kuboresha ufundishaji wa masomo ya lugha katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo. Hata hivyo, kuna changamoto ya mawasiliano inayotokana na uelewa mdogo wa lugha, mbinu duni, miundombinu na vifaa hafifu vya kufundishia na kujifunzia, upungufu wa walimu mahiri wa lugha, na matumizi madogo ya lugha za kigeni katika mawasiliano ya kawaida. Kwa kuzingatia ukubwa wa changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ya Kiswahili, Kiingereza, lugha nyingine za kigeni, LAT, Lugha ya Alama Mguso na maandishi ya Breli.

### Lengo

Kuimarisha matumizi ya lugha mbalimbali katika mawasiliano.

### Matamko

3.9.1. Serikali itahakikisha kuwa Kiswahili, Kiingereza na lugha nyingine za kigeni zinafundishwa kwa ufasaha na ufanisi katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

3.9.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itawezesha na kuendeleza Lugha ya Alama ya Tanzania, Lugha ya Alama Mguso, na maandishi ya Breli kutumika katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

## 3.10. Lugha ya Kufundishia

### Maelezo

Kwa kuwa ujuzi na maarifa huhifadhiwa na kusambazwa kupitia lugha fulani, lugha ya kufundishia ikitumika ipasavyo inaweza kuleta athari chanya katika matokeo ya ujifunzaji. Kwa sasa, lugha za kufundishia ni Kiswahili na Kiingereza nchini Tanzania. Lugha ya Kiswahili inatumika kufundishia elimu ya awali na msingi, na hufundishwa kama somo, wakati Kiingereza inatumika kama lugha ya kufundishia katika baadhi ya shule za msingi kwa utaratibu maalumu. Vilevile, lugha ya Kiingereza hutumika kufundishia katika shule za sekondari, vyuo vya ualimu ngazi ya stashahada, vyuo vya ufundi na vyuo vya elimu ya juu wakati Kiswahili kinafundishwa kama somo. Pia Kiswahili hutumika kama lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimu ngazi ya cheti, vyuo vya ufundi stadi na baadhi ya shule za sekondari inapohitajika.

Wakati huo huo, uzoefu kutoka nchi nyingine unadhihirisha umuhimu wa kutumia lugha inayotumiwa na wengi katika kujenga utambulisho na utamaduni wa nchi husika – mawasiliano ya kawaida. Kwa mantiki hiyo, upo umuhimu wa kusisitiza matumizi ya Kiswahili katika kufundishia masomo yanayojenga uelewa wa utamaduni na Historia ya Mtanzania ili kuihifadhi na kuitangaza. Aidha, Lugha ya Kiingereza ni nyenzo muhimu ya kuwezesha kupata maarifa. Hivyo, ni muhimu kutumia lugha zote mbili - Kiswahili kwa sababu kinaeleweka na wengi na Kiingereza kama chanzo cha maarifa katika kufundishia – kwani ni lugha tajiri.

### Lengo

Kutumia Lugha ya Kiswahili na Kiingereza katika ufundishaji na ujifunzaji.

### Matamko

*3.10.1. Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia katika elimu ya awali na elimu ya msingi, isipokuwa masomo ya lugha za kigeni na katika shule zitakazoomba na kuruhusiwa kutumia Lugha ya Kiingereza kufundishia.*

*3.10.2. Lugha ya Kiingereza itatumika kufundishia kuanzia ngazi ya sekondari ya chini (Kidato cha 1–4), isipokuwa somo la Kiswahili, masomo ya lugha za kigeni na katika shule za sekondari na vyuo vitakavyoruhusiwa kutumia Lugha ya Kiswahili kufundishia.*

*3.10.3. Lugha ya Taifa ya Kiswahili itatumika kufundishia masomo yenye lengo la kujenga na kuendeleza maadili, mila, desturi na utamaduni wa Mtanzania katika ngazi zote za elimu na mafunzo.*

## 3.11. Upimaji na Tathmini Katika Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Upimaji na tathmini husaidia katika kubaini maendeleo ya mwanafunzi na changamoto anazozikabili katika ujifunzaji. Aidha, upimaji unampa mwalimu fursa ya kutathmini tija katika ufundishaji na kufanya maboresho stahiki. Utaratibu wa sasa wa upimaji unazingatia upimaji endelevu na upimaji tamati katika ngazi zote za elimu. Hata hivyo, baada ya kuanzisha mitaala iliyolenga kujenga umahiri, utaratibu wa upimaji haukubadilishwa kuendana na mabadiliko hayo. Vilevile, msisitizo wa kujenga  stadi za karne ya 21 kama vile ubunifu, fikra tunduizi na utatuzi wa matatizo haukuwekwa bayana.

Kwa sababu hizo, Serikali imeona  umuhimu wa kuboresha mfumo wa upimaji kwa kutumia vigezo vinavyotambuliwa vya upimaji wa maendeleo ya kila siku ya mwanafunzi na tathmini ya mwisho ya kukamilisha ngazi ya elimu husika ili kuendana na mtaala unaozingatia ujenzi wa umahiri na kukuza stadi za karne ya 21

.

#### Lengo

Kuimarisha upimaji na tathmini ya maendeleo ya mwanafunzi.

#### Matamko

*3.11.1.1. Serikali itaendelea kuimarisha uwezo wa taasisi za upimaji na tathmini ya elimu na mafunzo.*

*3.11.1.2. Serikali itahuisha mfumo wa upimaji na tathmini kwa kuzingatia mtaala unaosisitiza ujenzi wa umahiri unaohitajika kwa kila ngazi ya elimu.*

## 3.12. Masuala ya Rasilimaliwatu

### 3.12.1. Upatikanaji wa Rasilimaliwatu katika Sekta ya Elimu

#### Maelezo

Uwepo wa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha ikiwemo walimu, wakufunzi na wahadhiri ni msingi wa utoaji wa elimu bora katika ngazi zote. Hii ndiyo sababu ya kwa nini Serikali imekuwa ikiongeza idadi na ubora wa rasilimaliwatu katika sekta ya elimu. Licha ya hayo, uhitaji wa rasilimali hizo katika shule za awali hadi sekondari umekuwa ukiongezeka mwaka hadi mwaka hususan katika masomo ya sayansi, lugha, hisabati na fani za amali. Pia, kuna upungufu mkubwa wa wakufunzi na wahadhiri katika taasisi za elimu ya amali na elimu ya juu.

Ili kuondokana na changamoto kama hizo, kuna umuhimu wa kuwa na mfumo wa kutambua mahitaji ya rasilimaliwatu katika kila ngazi ya elimu na mafunzo, na kuiandaa kulingana na vipaumbele vya Taifa. Pia, kuna umuhimu wa kuimarisha taratibu za ajira na mgawanyo wa rasilimaliwatu ili kukidhi mahitaji halisi katika kila taasisi na katika ngazi zote za elimu.

Kwa kuongezea, Serikali imeona kuwa kuna umuhimu wa kuweka mazingira bora yatakayohakikisha kwamba vijana wengi mahiri wanajiunga na kubaki katika fani ya ualimu, hususan katika masomo ya sayansi, hisabati, lugha na elimu ya amali. Pia, upo umuhimu wa kuwavutia na kuwabakiza kazini walimu, wakufunzi na wahadhiri mahiri ili kuinua ubora wa elimu, utafiti na huduma za jamii katika taasisi za elimu ya juu.

### Lengo

Kuwa na rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha katika ngazi zote za elimu.

### Matamko

*3.12.1.1. Serikali itaweka utaratibu wa kuandaa walimu na wakufunzi kulingana na vipaumbele na mahitaji ya Taifa katika ngazi husika.*

*3.12.1.2. Serikali itaweka mfumo fanisi wa mgawanyo wa walimu, wakufunzi na wahadhiri unaozingatia uhitaji katika kila eneo na kila ngazi.*

*3.12.1.3. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaweka mfumo fanisi wa kuwavutia na kuwabakiza walimu, wakufunzi na wahadhiri mahiri ikiwa ni pamoja na wanaofanya kazi katika mazingira magumu.*

*3.12.1.4. Serikali itaweka utaratibu wa utambuzi na usajili wa walimu na wakufunzi ili kukuza maadili, hadhi na kupanua fursa za ajira.*

*3.12.1.5. Serikali itaimarisha mfumo wa ajira ya walimu, wakufunzi, na wahadhiri kwa kuhakikisha kuwa wenye sifa na viwango stahiki wanaajiriwa baada ya kufanya mitihani na kufaulu kama sehemu ya usaili.*

*3.12.1.6. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha utoaji wa mafunzo kazini kwa walimu, wakufunzi na wahadhiri.*

*3.12.1.7. Serikali itaweka utaratibu wa kuwaandaa na kuwaendeleza wahadhiri kitaaluma kufikia viwango vyenye hadhi ya kimataifa kulingana na vipaumbele na mahitaji ya Taifa.*

*3.12.1.8. Serikali itaweka utaratibu wa kuongeza ushindani wa taasisi za elimu ya juu kwa kuwavutia na kuwabakiza wahadhiri wenye hadhi ya kimataifa kwa kuzingatia uwezo wao katika utafiti, machapisho na huduma za kitaalamu.*

### 3.12.2. Upatikanaji wa Rasilimaliwatu Mahiri kwa Ajili ya Sekta Nyingine

**Maelezo**

Uwepo wa uwiano mzuri wa rasilimaliwatu mahiri katika sekta zote za uchumi ni muhimu kwa maendeleo ya nchi. Kwa sababu hiyo, Serikali imeendelea kuongeza idadi na ubora wa rasilimaliwatu katika sekta zote kufikia kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano, katika miaka ya hivi karibuni, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka msisitizo katika kuongeza fursa za elimu ya msingi, sekondari na elimu ya juu. Hatua hiyo imesababisha ombwe la rasilimaliwatu katika kada ya kati, hususan wenye elimu ya amali, kukidhi mahitaji ya ongezeko hilo. Changamoto hii ilichagizwa na utaratibu wa kubadilisha baadhi ya taasisi za elimu ya kati kuwa vyuo vya elimu ya juu. Kwa muktadha huu, kuna umuhimu wa kujenga uwiano stahiki wa rasilimaliwatu yenye ujuzi katika fani mbalimbali, hususan zile zinazoakisi vipaumbele vya Taifa, Kikanda na Kimataifa.

**Lengo**

Kuwa na rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha kwa kukidhi mahitaji ya sekta nyingine.

**Matamko**

*3.12.2.1. Serikali itaweka utaratibu wa kufanya tathmini ya mara kwa mara ili kujua mahitaji halisi ya rasilimaliwatu katika sekta mbalimbali.*

*3.12.2.2. Serikali itaweka mazingira wezeshi kwa sekta ya elimu na mafunzo kuandaa rasilimaliwatu mahiri na ya kutosha kulingana na mahitaji ya Taifa.*

## 3.13. Menejimenti na Uendeshaji wa Elimu na Mafunzo

### 3.13.1. Uongozi, Usimamizi na Uendeshaji Fanisi Katika Sekta ya Elimu

#### Maelezo

Uongozi bora na usimamizi madhubuti wa sekta ya elimu ni muhimu ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo. Kwa sababu hiyo, Serikali imeendelea kuimarisha uongozi na usimamizi katika sekta ya elimu ikiwemo kuanzishwa na kuendelezwa kwa Wakala wa Uongozi wa Maendeleo ya Elimu (ADEM). Vilevile, Serikali imekuwa ikifanya mabadiliko ya viongozi pale inapoona inafaa ili kuimarisha uongozi, usimamizi na kuongeza tija katika sekta ya elimu.

Hata hivyo, bado kuna changamoto katika usimamizi na uendeshaji wa sekta ya elimu ikiwemo kufanyika kwa mabadiliko yasiyozingatia kikamilifu mahitaji na ushirikishwaji wa jamii. Pia, kuna mgongano wa baadhi ya sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayosimamia uendeshaji na utoaji wa elimu na mafunzo. Kwa mfano, katika uendeshaji, baadhi ya wadau wameonesha wasiwasi kuhusu utendaji wa baadhi ya viongozi katika sekta ya elimu. Hii inaashiria uwepo wa udhaifu katika sifa na uwezo wao kama viongozi. Kutokana na changamoto hizo, kuna umuhimu wa kuhuisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo inayohusu uendeshaji na usimamizi wa elimu na mafunzo. Vilevile, kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa mabadiliko yote makubwa katika sekta ya elimu yanatokana na tafiti za kisayansi na ushirikishwaji wa jamii. Pia, kuna umuhimu wa kuimarisha utaratibu wa kuwapata viongozi katika sekta ya elimu na kuhakikisha kuwa utaratibu huo unafuatwa.

#### Lengo

Kuimarisha uongozi, usimamizi na uendeshaji katika sekta ya elimu.

### Matamko

*3.13.1.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha mabadiliko ya kimkakati katika sekta ya elimu yanazingatia sheria, matokeo ya tafiti, mahitaji na ushirikishwaji wa wadau muhimu.*

*3.13.1.2. Serikali itahuisha sheria, taratibu, kanuni na miongozo, pamoja na muundo wa uongozi na usimamizi, ili kuwa na mfumo wa uendeshaji wa sekta ya elimu wenye tija.*

*3.13.1.3. Serikali itaimarisha utaratibu wa kuwapata na kuwaendeleza wasimamizi na viongozi wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.13.1.4. Serikali itahakikisha kwamba sheria za taasisi za elimu ya juu zinatekelezwa kikamilifu kwa kuzingatia majukumu yao ya msingi.*

## 3.13.2. Ushirikiano katika Elimu na Mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar

### Maelezo

Ushirikiano madhubuti kati ya Tanzania Bara na Zanzibar ni muhimu ili kuleta tija na ufanisi katika utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Kikatiba, elimu ya msingi, sekondari, ufundi na mafunzo ya ufundi stadi siyo masuala ya Muungano. Hata hivyo, elimu ya juu ni suala la Muungano. Lakini pia kuna ushirikiano wa karibu katika utekelezaji wa masuala mbalimbali ya elimu ikiwemo mitaala na upimaji kwa ngazi ya sekondari na elimu ya ufundi. Kwa kuzingatia hayo, kuna umuhimu wa kuendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano baina ya Tanzania Bara na Zanzibar katika utoaji wa elimu na mafunzo kwa ngazi zote ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa elimu ya juu.

### Lengo

Kuimarisha ushirikiano na uhusiano kati ya Tanzania Bara na Zanzibar katika masuala ya elimu na mafunzo.

### Tamko

*3.13.2.1. Serikali itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano katika elimu na mafunzo kati ya Tanzania Bara na Zanzibar.*

## 3.13.3. Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa katika Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Muingiliano wa kiuchumi, kisiasa na kijamii baina ya Tanzania, nchi marafiki na jumuiya za kikanda na kimataifa unatutaka kama nchi kuhakikisha kuwa tunatoa elimu na mafunzo yenye ubora na shindani. Hata hivyo, ingawa Tanzania imeridhia mikataba, itifaki na makubaliano mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo imechangia kuinua ubora wa elimu na mafunzo, bado zipo changamoto za kisera, kisheria, kimfumo, kimuundo na kijamii zinazopaswa kutatuliwa kwa lengo la kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo. Changamoto hizo zimesababisha baadhi ya itifaki, makubaliano na mikataba kusitishwa au kutotekelezwa kama ilivyokusudiwa. Hivyo, kuna umuhimu wa kutathmini na kuondoa vikwazo vinavyoathiri mahusiano ya kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.

### Lengo

Kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.

### Tamko

*3.13.4. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha uhusiano na ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika elimu na mafunzo.*

## 3.14. Upatikanaji wa Ardhi kwa Ajili ya Maendeleo ya Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Ili kuanzisha, kupanua na kuendeleza au kukarabati taasisi za elimu na mafunzi, ni lazima kutenga rasilimali-ardhi ya kutosha kukidhi mahitaji. Kwa upande mwingine, mahitaji ya ardhi kwa ajili ya taasisi za elimu na mafunzo yanaendelea kuongezeka

kutokana na azma ya Serikali kupanua fursa za elimu katika ngazi zote. Changamoto nyingine ni kwamba baadhi ya taasisi na asasi za elimu na mafunzo zimejengwa katika ardhi ambayo haina miliki ya kisheria. Aidha, wananchi wamekuwa wakivamia ardhi iliyotengwa kwa ajili ya baadhi ya taasisi za elimu na mafunzo. Kwa hali hiyo, taasisi za elimu na mafunzo zinahitaji kumilikishwa ardhi ya kutosha kwa mahitaji ya sasa na maendeleo ya baadaye. Hivyo, ni muhimu mipango ya ardhi ikatoa kipaumbele katika kutenga ardhi ya kutosha kwa mahitaji hayo kwa ngazi zote ikiwa ni pamoja na taasisi za elimu kuandaa mipango fanisi na endelevu ya matumizi ya ardhi zilizotengewa.

### Lengo

Kuwezesha upatikanaji wa ardhi kwa kuzingatia mahitaji kwa ajili ya matumizi ya elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.14.1. Serikali itahakikisha kuwa mahitaji ya ardhi kwa ajili ya elimu na mafunzo yanazingatiwa katika mipango ya maendeleo ya ardhi nchini.*

*3.14.2. Serikali itahakikisha kuwa inasimamia na kuzingatia ufanisi wa matumizi endelevu ya ardhi katika taasisi za elimu na mafunzo ngazi zote.*

## 3.15. Upatikanaji wa Taarifa na Takwimu Sahihi za Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Hatua zote za mipango ya elimu zinategemea uwepo wa taarifa na takwimu sahihi na zenye ubora, zilizochanganuliwa kwa kuzingatia vigezo vyote muhimu. Ili kuweza kupata taarifa na takwimu kwa urahisi ni muhimu kuwa na mifumo fanisi, salama, rafiki na unganifu. Hata hivyo, ingawa Serikali imeweka mifumo mbalimbali yenye taarifa na takwimu zinazohusu elimu na mafunzo, bado mifumo hiyo siyo unganifu. Kwa upande mwingine, usahihi wa baadhi ya taarifa na takwimu una changamoto kutokana na tofauti zilizopo katika ukusanyaji, uhakiki, uchambuzi na uhifadhi wake. Kwa muktadha huo, kuna umuhimu wa kuwa na mfumo madhubuti wa kukusanya, kuhakiki, kuchambua, kuhifadhi na kusambaza takwimu na taarifa

zote muhimu zinazohusu sekta ya elimu. Pia, kuna umuhimu wa kurahisisha na kuimarisha upatikanaji wa taarifa zinazohusu elimu na mafunzo kwa kutumia tafiti za kisayansi hasa kwa njia unganishi za kiteknolojia.

### Lengo

Kuwa na mfumo unganifu wa taarifa na takwimu katika sekta ya elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.15.1. Serikali itahakikisha uwepo wa mfumo unganifu wa taarifa na takwimu zinazohusu elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.15.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha ufanyaji wa tafiti na utekelezaji wa matokeo ya tafiti hizo katika kuinua ubora wa elimu na mafunzo nchini.*

## 3.16. Ugharamiaji Endelevu wa Elimu na Mafunzo

### Maelezo

Katika kutimiza azma ya Serikali ya kuwa na Taifa la watu walioelimika, ni muhimu kuwa na mfumo fanisi na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, imekuwa ikigharamia elimu na mafunzo katika ngazi zote. Hata hivyo, licha ya ongezeko la bajeti la mwaka hadi mwaka, bado kuna changamoto katika ugharamiaji wa elimu na mafunzo nchini kutokana na ongezeko la mahitaji. Changamoto nyingine ni pamoja na fedha zinazotengwa katika bajeti ya Serikali kutotosheleza mahitaji na hivyo kuathiri fursa za upatikanaji wa elimu na ubora ake. Kwa sababu hiyo, kuna umuhimu wa kuweka mfumo wenye vyanzo anuai na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo.

### Lengo

Kuwa na mfumo endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.16.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaendelea kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu katika ngazi zote.*

*3.16.2. Serikali itahakikisha kuwa ada na michango katika ngazi mbalimbali za elimu inazingatia hali halisi ya uchumi, huduma zinazotolewa na taasisi, na misingi ya elimu bora na endelevu wa uwekezaji katika sekta mbalimbali.*

## 3.17. Masuala Mtambuka katika Elimu na Mafunzo

### 3.17.1. Elimu ya Afya ya Mazingira

### Maelezo

Elimu ni moja ya nyenzo muhimu katika utoaji wa huduma bora za afya na kuhakikisha uwepo wa mazingira salama kwa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Kinyume na hilo, ongezeko la idadi ya watu na shughuli mbalimbali za kijamii na za kiuchumi yamechangia katika uharibifu wa mazingira nchini. Hivyo ni muhimu kuendelea kuimarisha utoaji wa elimu ya afya ya mazingira katika ngazi zote za elimu kwa lengo la kujenga utamaduni wa kutunza mazingira.

### Lengo

Kuwa na wahitimu katika ngazi zote za elimu na mafunzo wenye uelewa na kuthamini afya na umuhimu wa kutunza mazingira.

### Tamko

*3.17.1.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha kuwa maudhui kuhusu elimu ya afya ya mazingira hasa mabadiliko ya tabianchi yanazingatiwa katika mitaala ya elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

### 3.17.2. Magonjwa na Majanga

#### Maelezo

Sekta ya elimu ni mojawapo ya sekta nyingi zinazoathiriwa na magonjwa na majanga mbalimbali. Athari hizo zinasababisha kushuka kwa ubora wa elimu kutokana na vifo na mahudhurio duni ya wanafunzi, walimu, wakufunzi na wahadhiri. Licha ya mitaala katika ngazi zote kusisitiza utoaji wa elimu ya afya na kujikinga na majanga, bado wahusika tajwa hawana uelewa wa kutosha wa kukabiliana na magonjwa na majanga. Kwa sababu hizo, Serikali imeona umuhimu wa kuimarisha elimu kuhusu kujikinga na magonjwa na kukabiliana na majanga mbalimbali.

#### Lengo

Kuimarisha utoaji wa elimu kuhusu majanga na magonjwa mbalimbali yanayoambukiza na yasiyoambukiza katika ngazi zote za elimu na mafunzo.

#### Matamko

*3.17.2.1. Serikali itajumuisha stadi za kukabiliana na majanga na kujikinga na magonjwa mbalimbali katika mitaala ya elimu na mafunzo kwa ngazi zote kwa kuzingatia mahitaji ya wakati husika.*

*3.17.2.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itahakikisha inaweka utaratibu wa kuendelea kutoa elimu na mafunzo wakati wa majanga na magonjwa ya mlipuko.*

## 3.18. Utafiti na Maendeleo ya Sekta ya Elimu

#### Maelezo

Misingi ya utoaji na uendelezaji wa elimu na mafunzo pamoja na utatuzi wa changamoto za jamii unategemea matokeo ya tafiti mbalimbali, ushirikishwaji wa jamii na wadau wa sekta ya elimu. Tafiti zinaonesha kuwa nchi za Afrika, ikiwemo Tanzania, zimekuwa zikifanya mabadiliko katika sekta ya elimu bila kufanya tafiti au kuzingatia taratibu zinazoongoza namna bora ya kuendeleza elimu na mafunzo.

Hata hivyo, tangu kupata uhuru, sekta ya elimu nchini Tanzania imepitia mabadiliko mbalimbali ambayo yalilenga kuendeleza elimu na mafunzo na kutoa mchango stahiki katika maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Ingawa mabadiliko hayo yanapaswa kuzingatia tafiti, kiasi kidogo cha fedha zinazotengwa kwa ajili ya tafiti katika sekta ya elimu hapa nchini kimesababisha tafiti kuwa chache na kufanyika kwa kutegemea hali ya upatikanaji wa rasilimali kutoka kwa wadau wa maendeleo wa ndani na nje.

#### Lengo

Kuwezesha ufanyikaji wa tafiti na matumizi ya matokeo yake katika kuendeleza elimu na mafunzo nchini.

#### Matamko

*3.18.1. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaziwezesha na kuimarisha tafiti za kielimu na matumizi ya matokeo yake katika ngazi zote za elimu na mafunzo nchini.*

*3.18.2. Serikali, kwa kushirikiana na wadau, itaimarisha na kuhamasisha taasisi za elimu ya juu kufanya tafiti na kusimamia matumizi ya matokeo yake katika kuinua ubora wa huduma za jamii nchini.*

### 3.19. Ushirikiano wa Sekta ya Umma na Binafsi katika Utoaji wa Elimu na Mafunzo

#### Maelezo

Elimu ni mojawapo ya eneo muhimu la ushirikiano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ambapo sekta binafsi, kama ilivyo kwa umma, inashiriki kutoa elimu na mafunzo katika ngazi zote. Hata hivyo, licha ya mchango mkubwa wa Serikali katika utoaji wa elimu, umuhimu wa kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika jukumu hili ni mkubwa sana kutokana na ongezeko la mahitaji. Aidha, ni muhimu kuimarisha ushirikishwaji wa wadau wote muhimu, ikiwemo wazazi na jamii, katika utoaji wa elimu. Kwa sababu hiyo, ni muhimu kwa Serikali kuweka mazingira wezeshi ili kuivutia sekta binafsi na wadau wengine kuongeza ushiriki wao katika utoaji wa elimu na mafunzo.

### Lengo

Kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi na wadau wengine katika utoaji wa elimu na mafunzo.

### Matamko

*3.19.1. Serikali itaimarisha ubia baina ya sekta ya umma, sekta binafsi na wadau wengine katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

*3.19.2. Serikali itaimarisha ushirikishwaji wa wadau mbalimbali katika utoaji wa elimu na mafunzo katika ngazi zote.*

# SURA YA NNE

## MUUNDO WA KISHERIA

### 4.1. Utangulizi

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023, utazingatia mfumo wa kisheria utakaowezesha wahusika kutekeleza majukumu yao ipasavyo. Matamko ya Sera yanapata nguvu yake ya utekelezaji kutokana na sheria na kanuni zake.

### 4.2. Sheria za Kusimamia Elimu na Mafunzo

Katika kutekeleza Sera hii, baadhi ya sheria zinazotumika sasa zitabaki kama zilivyo na nyingine kufanyiwa marekebisho. Sheria zinazoweza kufanyiwa marekebisho ili kuendana na mahitaji ya sera mpya ni kama zifuatazo:

#### 4.2.1. Mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353

Sheria hii pamoja na masuala mengine itarekebishwa katika maeneo yafuatayo:

a. Kubainisha umri wa kuanza elimu ya awali na muda wake;
b. Kubainisha umri wa kuanza elimu ya msingi na muda wake;
c. Kutambua elimu ya lazima katika mfumo wa elimu;
d. Kutambua mikondo ya elimu ya jumla na elimu ya amali katika mfumo wa elimu na mafunzo;
e. Kubainisha lugha ya kufundishia katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo;
f. Kubainisha utaratibu wa uteuzi, majukumu na mamlaka ya uwajibikaji wa wathibiti ubora wa shule na Maafisa Elimu kwa ngazi mbalimbali; na
g. Kuitambua dhana ya uthibiti ubora wa elimu katika mfumo wa elimu na mafunzo.

### 4.2.2. Mapitio ya Sheria Mbalimbali za Taasisi Zilizo Chini ya Wizara yenye Dhamana ya Elimu

Sheria mbalimbali za taasisi zilizo chini ya wizara yenye dhamana ya elimu zitafanyiwa mapitio ili:

a. kubainisha majukumu pamoja na masharti mengine kuendana na mahitaji ya sasa ya Sera;

b. kuondoa migongano/mfanano wa majukumu kati ya taasisi moja na nyingine; na

c. kuweka utaratibu wa kuhusiana kiutendaji kati ya taasisi moja na nyingine hususan kwa taasisi zile ambazo majukumu yao yanategemeana.

Sheria za taasisi zitakazofanyiwa mapitio ni pamoja na:

i. Sheria ya Baraza la Mitihani la Tanzania, Sura 107;

ii. Sheria ya Taasisi ya Elimu Tanzania, Sura 142;

iii. Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, Sura 178;

iv. Sheria ya Vyuo Vikuu, Sura 346;

v. Sheria ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 129;

vi. Sheria ya Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Sura 82;

vii. Sheria ya Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania, Sura 102;

viii. Sheria ya Mfuko wa Elimu, Sura 412; na

ix. Sheria ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Sura 139.

### 4.2.3. Mapitio ya Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Wilaya), Sura 287 na Sheria ya Serikali za Mitaa (Mamlaka za Miji), Sura 288

Sheria za Serikali za mitaa zitafanyiwa mapitio ili:

a. Kubainisha majukumu yanayohusiana na usimamizi na uendeshaji wa elimu katika mamlaka za Serikali za mitaa kuendana na mahitaji ya sasa ya utekelezaji wa Sera;

b. Kuondoa migongano/mifanano ya kimajukumu ya usimamizi na uendeshaji wa elimu kati ya mamlaka za Serikali za mitaa na mamlaka zingine za Serikali; na

c. Kuweka utaratibu wa kuhusiana kiutendaji kati ya mamlaka za Serikali za mitaa na mamlaka nyingine za Serikali kuhusiana na usimamizi na uendeshaji wa elimu katika maeneo yao.

# SURA YA TANO

## MUUNDO WA KITAASISI, UFUATILIAJI NA TATHMINI

### 5.1. Muundo wa Kitaasisi

Utekelezaji wa Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023 utazingatia muundo mahsusi wa kitaasisi katika ngazi mbalimbali kuanzia ngazi ya Taifa hadi ngazi za chini kwa kufuata mgawanyo wa majukumu kama ilivyooneshwa katika sehemu zifuatazo:

### 5.2. Ngazi ya Taifa

#### 5.2.1. Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Mafunzo

Majukumu ya wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo ni:

(i) Kutunga Sera ya Elimu na Mafunzo kwa ngazi zote;

(ii) Kuandaa mipango na programu za utekelezaji wa Sera;

(iii) Kubuni, kutekeleza na kutathmini miradi mbalimbali kwa ajili ya kufikia malengo ya Sera;

(iv) Kuweka viwango vya ubora wa elimu na mafunzo na kusimamia uzingatiaji wake katika kufikia malengo ya Sera;

(v) Kuandaa muundo fanisi wa kitaasisi kwa ajili ya utekelezaji wa sera na kumwezesha waziri mwenye dhamana ya elimu kusimamia maendeleo ya elimu na mafunzo nchini;

(vi) Kujenga uwezo wa wizara, taasisi na vyombo vilivyo chini ya wizara kwa ajili ya kutekeleza sera;

(vii) Kutoa miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa sera kwa kuzingatia matokeo ya tathmini, tafiti na taarifa mbalimbali zinazohusu utoaji wa elimu na mafunzo; na

(viii) Kuratibu utekelezaji, ufuatiliaji na tathmini ya sera, mipango, na programu mbalimbali za uendelezaji wake.

Katika utekelezaji wa sera, sheria, kanuni, miongozo na taratibu za utoaji wa elimu na mafunzo, wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo itazishirikisha wizara nyingine, taasisi na wadau wa elimu na mafunzo nchini.

### 5.2.2. Wizara yenye Dhamana ya Elimu na Sekta Nyingine

Wizara yenye dhamana ya elimu itashirikiana na wizara na taasisi mbalimbali zenye dhamana zinazowezesha utoaji wa Elimu na Mafunzo nchini. Wizara hizo kulingana na majukumu yake zitasaidia kupatikana kwa huduma stahiki za utoaji wa elimu na mafunzo. Aidha, wizara yenye dhamana ya elimu itaweka utaratibu wa mawasiliano ili kuhakikisha utekelezaji wa sera unazingatia utaratibu na miongozo mbalimbali. Wizara hizo ni pamoja na:

*(a) Wizara yenye Dhamana ya Fedha*

Wizara yenye dhamana ya fedha itakuwa na jukumu la kuwezesha upatikanaji wa rasilimalifedha kwa ajili ya ugharamiaji wa Sera katika ngazi zote. Aidha, itahusika na utoaji wa sera za jumla za kiuchumi, miongozo na mipango ya fedha na takwimu.

*(b) Wizara yenye Dhamana ya Utumishi wa Umma*

Wizara yenye dhamana ya utumishi wa umma itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu utawala wa utumishi wa umma, mikataba ya utendaji kazi, maslahi na mipango ya maendeleo ya rasilimaliwatu na maadili ya utumishi wa umma katika sekta ya elimu.

*(c) Wizara yenye Dhamana ya Teknolojia ya Habari*

Wizara yenye dhamana ya teknolojia ya habari itakuwa na jukumu la utekelezaji wa mkakati kwa kutoa miongozo ya TEHAMA, uendelezaji wa mifumo yake na usalama wa mifumo hiyo.

*(d) Wizara yenye Dhamana ya Ardhi*

Wizara yenye dhamana ya Ardhi itakuwa na jukumu la utekelezaji wa Mkakati kwa kutoa Miongozo ya maendeleo ya ardhi kwa shughuli za elimu na mafunzo; uthamini wa ardhi na hatimiliki za ardhi kwa maendeleo ya elimu na mafunzo nchini.

*(e) Wizara yenye Dhamana ya Afya*

Wizara yenye dhamana ya Afya itakuwa na jukumu la ukaguzi wa huduma za afya

na kutoa miongozo kuhusu kinga na tiba, chakula na lishe itakayozingatiwa na taasisi za elimu na mafunzo.

*(f) Wizara yenye Dhamana ya Utamaduni*

Wizara yenye dhamana ya utamaduni itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu uhamasishaji na uendelezaji wa utamaduni katika taasisi za elimu na mafunzo.

*(g) Wizara yenye Dhamana ya Michezo*

Wizara yenye dhamana ya michezo itakuwa na jukumu la kutoa miongozo kuhusu uhamasishaji na uendelezaji wa michezo katika taasisi za elimu na mafunzo.

*(h) Ofisi yenye Dhamana ya Uandishi wa Sheria*

Ofisi yenye dhamana ya uandishi wa sheria itakuwa na jukumu la kutekeleza mkakati kwa kuandika sheria mpya au/na kurekebisha sheria zilizopo ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati.

*(i) Wizara yenye Dhamana ya Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa*

Wizara yenye dhamana ya ushirikiano wa kikanda na kimataifa itakuwa na jukumu la utekelezaji wa mkakati kwa kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya elimu katika kuandaa, kuhuisha na kutekeleza mikataba na itifaki mbalimbali za kuwezesha uimarishaji wa ushirikiano wa kikanda na kimataifa katika masuala ya elimu na mafunzo.

*(j) Wizara yenye Dhamana ya Maendeleo ya Mtoto*

Wizara yenye dhamana ya maendeleo ya mtoto itakuwa na jukumu la kushirikiana na Wizara yenye dhamana ya elimu katika uwianishaji wa malezi na makuzi ya mtoto yatolewayo katika vituo vya kulelea watoto na elimu ya awali.

### 5.2.3. Wadau wa Maendeleo

Wadau wa Maendeleo watakuwa na jukumu la kutenga na kutoa rasilimali ili kuwezesha utekelezaji wa Sera hii; kushiriki katika shughuli mbalimbali zinazolenga kuongeza fursa na kuinua ubora wa elimu na kuwajengea uwezo wadau mbalimbali wanaotekeleza afua za utoaji wa elimu na mafunzo nchini.

### 5.2.4. Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia

Sekta Binafsi na Asasi za Kiraia watakuwa na jukumu la kutekeleza Sera kwa kushiriki katika ujenzi wa shule na Vyuo, kuchangia katika ujenzi wa miundombinu, uzalishaji wa nyenzo, zana na vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

### 5.2.5. Taasisi na Mamlaka Mbalimbali za Kusimamia Utoaji wa Elimu na Mafunzo

Taasisi na mamlaka za usimamizi wa elimu na mafunzo zitakuwa na jukumu la kutoa ithibati, kuthibiti na kusimamia masuala mbalimbali ya elimu na mafunzo nchini kulingana na majukumu yake kama yatavyoainishwa kisheria. Mamlaka hizo zitakuwa huru na zenye kauli ya mwisho, isipokuwa pale tu zitakapoelekezwa vinginevyo na waziri mwenye dhamana ya elimu na mafunzo. Wakati huo huo, mamlaka hizo zitashirikiana kwa karibu na wizara, idara, taasisi na wadau wote muhimu katika kutekeleza majukumu yao.

### 5.2.6. Taasisi na Bodi Mbalimbali za Kitaalamu

Taasisi na bodi zenye wajibu na masuala mbalimbali ya kitaalamu zitawajibika kusimamia masuala ya utaalamu baada ya wanafunzi kumaliza masomo yao kwenye taasisi za elimu na mafunzo husika. Vilevile, taasisi na bodi hizo zitawajibika kuzishauri mamlaka mbalimbali zinazosimamia utoaji wa elimu na mafunzo nchini katika masuala ya viwango vya elimu na mafunzo yatolewayo. Hata hivyo, taasisi na bodi za kitaalamu hazitakuwa na mamlaka ya moja kwa moja ya kutoa maelekezo kwenye taasisi za elimu na mafunzo isipokuwa kwa kupitia kwenye mamlaka rekebu za taasisi hizo.

### 5.2.7. Ngazi ya Mkoa

Jukumu la usimamizi wa utekelezaji wa Sera katika ngazi ya mkoa litakuwa la

Afisa Elimu wa Mkoa (REO) husika. REO atakuwa na jukumu la kutoa taarifa na ushauri kwa mamlaka husika kuhusu utekelezaji wa sera na maendeleo ya elimu na mafunzo katika ngazi hiyo.

### 5.2.8. Ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa

Jukumu la usimamizi na utekelezaji wa Sera katika ngazi ya halmashauri litakuwa la Mamlaka za Serikali za Mitaa chini ya usimamizi wa Afisa Elimu husika. Afisa elimu atakuwa na jukumu la kuandaa mipango na bajeti, na kusimamia uendeshaji wa shule za elimu ya awali, msingi na sekondari kwa kuzingatia maelekezo ya sera. Afisa elimu husika atakuwa na jukumu la kutoa taarifa na ushauri kwa mamlaka zinazohusika na utekelezaji wa sera na maendeleo ya elimu na mafunzo katika ngazi hiyo.

Pia, mamlaka za serikali za mitaa zitahusika katika uanzishaji, usimamizi na uendeshaji wa shule za elimu ya awali, msingi, sekondari, vituo vya elimu ya watu wazima na elimu nje ya mfumo rasmi katika maeneo wanayosimamia kulingana na maelekezo ya sera. Vilevile, zitawajibika kutoa taarifa ya utekelezaji wa sera kwa mamlaka husika.

Kwa kuongezea, mamlaka za Serikali za mitaa zitasimamia utekelezaji wa sera kwa kufuata sheria, kanuni, miongozo na taratibu za usimamizi na uendeshaji wa shule za Serikali na zisizo za Serikali. Katika kutekeleza jukumu hilo, mamlaka zitatakiwa kushirikiana na wakuu wa shule za msingi na sekondari za Serikali na zisizo za Serikali, na mashirika na taasisi za Serikali na zisizo za Serikali katika ngazi hizo. Vilevile, Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa sera ya elimu na mafunzo zitawajibika kutoa taarifa katika mamlaka husika ya usimamizi wake.

### 5.2.9. Shule na Vyuo

Wakuu wa shule na vyuo watasimamia na kutekeleza sera ya elimu na mafunzo kwa kuzingatia maelekezo ya sera yenyewe. Pia, watawajibika kutoa taarifa za utekelezaji wa sera katika taasisi zao za usimamizi na kwa mamlaka husika.

### 5.2.10. Jamii na Wazazi/Walezi

Wazazi na walezi ni wadau muhimu katika kuimarisha maendeleo ya elimu kwa mwanafunzi. Ili kufanikisha hilo, ushirikiano kati ya mzazi/mlezi na walimu au uongozi wa shule ni muhimu. Majukumu ya mzazi na mlezi ni pamoja na kuhakikisha upatikanaji wa huduma stahiki kwa mwanafunzi kama vile mavazi, chakula na lishe, malazi, vifaa vya kujifunzia, ulinzi na usalama. Aidha, ni jukumu la mzazi/mlezi kufuatilia nidhamu, maadili na mwenendo wa kitabia wa mtoto wake.

## 5.3. Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ni jukumu la wizara yenye dhamana ya elimu na mafunzo kwa kushirikiana na wadau. Wizara itapokea taarifa ya utekelezaji wa Sera kama ilivyofafanuliwa katika Mkakati wa Utekelezaji wa Sera kutoka kwa watekelezaji. Pia, wizara ina jukumu la kukusanya, kuchambua, na kuunganisha taarifa za utekelezaji wa sera kutoka kwa wadau mbalimbali wa sekta ya umma na binafsi. Wadau hao watawajibika kutoa taarifa stahiki kwa wizara husika ili kufanikisha ufuatiliaji na tathmini ya maendeleo ya utekelezaji wa Sera. Kwa upande mwingine, wizara itaandaa mpango wa ufuatiliaji na tathmini ya Sera ambao utaonesha viashiria, vigezo na muda wa tathmini kwa kuzingatia mkakati wa utekelezaji wa Sera.

## 5.4. Hitimisho

Madhumuni ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014 Toleo la 2023 ni kutoa mwongozo wa jumla wa utekelezaji wa afua mbalimbali katika maeneo yenye vipaumbele kwa kushirikisha sekta ya umma na wadau wengine. Katika utekelezaji wa malengo ya Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Serikali ilitekeleza mikakati mbalimbali iliyowezesha upatikanaji wa mafanikio makubwa katika utoaji wa elimu na mafunzo nchini. Mafanikio hayo ni matokeo ya ushirikiano wa wadau mbalimbali wakiwemo wazazi, jamii, sekta za umma na binafsi na wadau wengine wa maendeleo. Pamoja na mafaniko hayo, hali ya utoaji wa elimu haijafikia kiwango kilichokusudiwa.

Kwa muktadha huo, Sera ya Elimu na Mafunzo 2014, Toleo la 2023 inalenga kutatua changamoto kuu saba katika utoaji wa elimu na mafunzo ambazo ni: mfumo wa elimu kujikita zaidi kwenye elimu ya jumla na kukosa fursa anuai za elimu na mafunzo kwa kuzingatia mahitaji, njia mbalimbali za ujifunzaji kulingana na mazingira; mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu na mafunzo kutokidhi mahitaji ya mabadiliko ya kiuchumi, kijamii, kisayansi na kiteknolojia; kuwa na mfumo usio fanisi wa uthibiti na ithibati ya elimu na mafunzo katika ngazi zote; upungufu wa nguvukazi ya kutosha yenye maarifa, stadi na ujuzi unaohitajika kwa ajili ya sekta mbalimbali; mfumo dhaifu wa usimamizi na uendeshaji wa elimu na mafunzo; mfumo usio wa uhakika na endelevu wa ugharamiaji wa elimu na mafunzo wenye vyanzo anuai na endelevu; na kutozingatiwa kwa masuala yanayoibuka ambayo yanaathiri utoaji wa elimu na mafunzo.

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.
Mji wa Serikali, Eneo la Mtumba,
Mtaa wa Afya,
S. L. P. 10,
40479 DODOMA.
Barua pepe: info@moe.go.tz
Tovuti: www.moe.go.tz

moestvt wizara_elimuTanzania wizara_elimutz elimutz elimutalktz